

KWA NINI?



Asante sana Ndugu Ernie. Ni, nayahesabu haya kuwa ni majaliwa mengine makuu kuwa hapa kwenye, ukumbi huu usiku wa leo, kuninii, katika utumishi wa Bwana.

² Na sasa, kesho usiku ni usiku maalum wa maombi kwa ajili ya wagonjwa, kwa kuwa, ninaamini wanautoa zaidi kwa watu ambao ni, wata—watakaokuja kutoka hospitalini na kadhalika.

³ Kwa kawaida mikutanoni tunapoiandaa, tuna chu—chumba cha dharura ambacho, wanapokuwa na mkutano mkubwa, mahali walipokuwa, watu wanaweza kuingia na kuombewa, kila wakati wanapokuja ambao hawawezi kuingia kwenye mstari wa maombi. Tuna chumba ambacho. . . Labda wamekuja, wakaruka kwa ndege, ama chochote kile, kwa mamia ya maili, na inabidi tu kuwa huko usiku huo mmoja, kisha warudi. Kwa hiyo, daima tunajaribu kuwashika wote. Lakini wakati tunapokuwa na ibada ya namna hii, ni—ninajisikia ya kwamba kila mtu aliye humu jengoni *ameombewa* kila usiku, mnaona, kwa sababu, kama vile ninavyojaribu kulifanya dhahiri, mnaona, kwamba—kwamba kama kulikuwa na. . .

⁴ Ni—ni. . . Mnaona, kama vile mtu aliyeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu. Kama nilijua ya kwamba kuna. . . Kama ningeweza kuchukua sarafu ya robo na kuisukuma kwa pua yangu kuzunguka mji huu, kumfanya mtu huyo ainuke kutoka kwenye kiti hicho, na aponywe, ningefanya hivyo. Hakika, bila shaka ningefanya hivyo. Na sasa, labda ataishi maisha ya kawaida ameketi katika kiti hicho. Lakini labda kuna mtu aliyeketi huko nje, mahali fulani, ambaye ana ugonjwa wa moyo, na saa chache tu kuanzia sasa atakuwa amekufa, isipokuwa Kitu fulani kimsaidie, yuko katika hali mahututi zaidi, kuliko mtu huyu aliyeketi kitini. Ndipo ningesukuma hiyo robo, bila shaka, kuzunguka mji kwa pua yangu, ambako kungenichukua siku nyingi kufanya hivyo, lakini, na labda nisingekuwa na pua iliyosalia nilipomaliza kuisukuma kote, bali ningefanya hivyo nipate kumwona maskini mwanadamu huyo ameponywa.

⁵ Kwa hiyo, si—siwezi kumponya mtu yeyote, sijawahi kumponya mtu yeyote, bali nimeona makumi elfu wakiponywa. Na kwa hiyo, mimi. . . kama. . . jambo pekee ninalojaribu kufanya ni kuwafanya wawe na imani katika yale ambayo tayari yametengwa kwa ajili yao. Kwa hiyo, mnapoona. . .

⁶ Hebu wazieni tu, kama Yesu alikuja hapa usiku wa leo, na alikuwa amevaa suti hii aliyonipa, nawe ungemwendea na kusema, “Bwana, utaniponya?”

Yeye, labda, angekuangalia kwa mshangao sana, angesema, “Unaniamini Mimi? Hivi huyasomi Maandiko?”

“Naam, Bwana.”

“Vema, hivi hukusoma ambapo nilinunua uponyaji wako pale Kalvari?” Unaona? “Tayari nimefanya hivyo, ninii Yangu...”

⁷ Kama wewe, jambo ndilo hili hapa, kama umewahi kuona kitu chochote katika duka la rehani, halafu uende na kukomboa hicho kutoka kwenye hilo duka la rehani, huwezi kukikomboa mara ya pili, tayari kimekombolewa. Mtu akikupa tiketi ambapo gharama imelipwa, na bidhaa hiyo imekombolewa, imekombolewa, haikubidi kuilipia mara ya pili.

⁸ Hapo ndipo Musa alipotenda dhambi yake kwa kuupiga ule Mwamba mara ya pili, badala ya kuuzungumzia. Mnaona? Yeye aliupiga mara ya kwanza. Ilinena juu ya nini? Udhaifu wa Damu ya Yesu ambapo ingembidi kupigwa kwa ajili ya kila mtu binafsi. Kristo alipigwa kwa ajili ya uponyaji wetu, tunasema tu na Mwamba sasa, nao unaleta uponyaji Wake.

⁹ Lakini, mnaona, tumefundisha vibaya, yote kuhusu huku kuwekea mikono, na mihemko, na... Kamwe usijenge matumaini yako—yako ya wokovu juu ya mhemko, maana unaweza kuwa na mihemko ya kila namna, bali ujenge juu ya Neno la Mungu, hapo ndipo unapoweza kumshinda Shetani wakati wowote, juu ya Neno, ni BWANA ASEMA HIVI.

¹⁰ Ninakumbuka usiku mmoja... Sitaki kuwaweka hapa kama... Sitasema lolote usiku wa leo, tulieni tu. Nilikuwa... Mambo mengi sana ambayo kama ningeweza kukaa hapa kwa mwezi mmoja, ambayo ningeweza nusu, nisingeweza kusimulia nusu yake. Kama ningeweza kuandika katika vitabu yale niliyomwona Bwana akifanya, karibu yangejaza maktaba yenyewe. Mamia ya vitabu hayangeandika mambo ambayo nimeona, ku—kujua tu Yeye aliyafanya, katika miaka hii ipatayo thelathini na mitano, ama, miaka thelathini na mmoja, ndivyo ilivyo, ya utumishi Kwake, ambayo nimemwona akifanya katika mikutano ambayo nimefanya, na kote ulimwenguni. Na yale mambo makuu, ilikuwa ni ya kushangaza kwamba ilininii. . .

¹¹ Vema, ninaweza kuyakumbuka, na kuyawazia, bali hatuyaandiki tunayaachilia tu, kwa sababu wakati mwingine Yesu alisema, “Angalieni msimwambie mtu yeyote.” Mnaona? Hata hivyo, Yesu alikufa kwa ajili ya watu ambao Mungu alitangulia kujua wangeokolewa, mnaona. Sasa, hiyo ni kweli. Yeye alikuja kuokoa kile kilichopotea, bali kwa kujua Kwake tangu zamani Yeye alijua ni nani angeokolewa. Sasa, uponyaji, bila shaka, ni kwa ajili ya kila mtu aliye na imani ya kutosha kuupokea; wokovu ni kwa kila mtu aliye na imani ya kutosha kuupokea.

¹² Katika mkutano mmoja, kama sijakosea, ilikuwa ni papa hapa Illinois. Hivi kuna mahali padogo hapa panapoitwa Vandalia ama kitu fulani? Vanda-... Van-... Naamini hapo

ndipo ilipokuwa, Vandalia, ama—ama ng'ambo tu ya mto huko Missouri. Ilikuwa mahali fulani hapa, ninaamini, huku Illinois, kulikuwako na mama mmoja akipitia mstarini usiku mmoja.

¹³ Nawe inakubidi kuangalia yale Yeye asemayo. Sasa, katika maono haya mnayoyaona hapa yakitukia jukwaani, sifanyi hivyo. Mnajua ni nani anayefanya hivyo? Wewe unalifanya. Hujui, bali wewe ndiwe unayelifanya. Unasema, "Ndugu Branham!" Hiyo ni kweli kabisa, enyi darasa. Unafanya hivyo mwenyewe. Hiyo ni ninii tu... Laiti ningaliweza kulielezea lakini hakuna njia ya kulielezea. Ni kama tu kubadilisha gari lako na kuliingiza gia. Unaona? Na kama tu, Roho Mtakatifu, karama tu ya kujua jinsi ya kujiondoa mwenyewe, na kumwacha Yeye azungumze. Mnaona, kujiondoa, ndipo si wewe unayezungumza, ni Yeye. Nawe unafanya hivyo mwenyewe.

¹⁴ Kujaribu kufanya mshangao kidogo juu yake, ningesema... maelezo, ningesema hivi: Labda sote—sote tunaenda kwenye kanivali, kuna kanivali hii inayokuja mjini, sarakasi. Nasi sote tuko hapa juu, sisi wahudumu, sisi ni—sisi ni jamaa wachanga, nasi hatutaingia kuiona hiyo. Kwa hiyo ilitokea kwamba nilikuwa jamaa mkubwa mno, mrefu, mwembamba, na ndugu, hapa, alikuwa mfupi na mwenye nguvu. Sasa, huenda akawa na nafasi bora zaidi ya... Yeye ana nguvu kuniliko, vema sasa, angeweza kubeba maji, ni mkubwa, ana nguvu, angeweza kufanya mambo ambayo nisingeweza kufanya kamwe. Sasa, siwezi kujizuia kwa sababu ningekuwa mrefu na mwembamba, yeye hawezi kujizuia kwa sababu yeye ni mfupi na mwenye nguvu. Mnaona? "Ni yupi, akijisumbua, aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja?" alisema Yesu. Tuko kile tulicho.

¹⁵ Na hilo ndilo jambo moja ambalo limeathiri uamsho wetu wa Kipentekoste, na miamsho mingine, ni mtu fulani anayejaribu kuwa kitu ambacho wasicho, wanajaribu kumwiga mtu mwingine. Huwezi kufanya hivyo, uko tu kile ulicho, hivyo tu. Na unapofanya hivyo, Mungu atakutumia tu jinsi ulivyo.

¹⁶ Nawe ni muhimu tu kama mtu mwingine yeyote. Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, ile springi iliyu ndogo sana katika saa hii ni muhimu tu kama ile springi kuu, maana zote zinahitajika kwa kupima wakati. Na hivyo... Tunapotambua mahali petu katika Kristo, na kisha kudumu hapo, kama ni maskini mke wa nyumbani, kaa papo hapo, hivyo ndivyo Mungu anavyokutaka ufanye. Unaona? Kuwa tu kile ulicho.

¹⁷ Na wengi wenu mnakumbuka kuponywa kwa Mbunge Upshaw, alikuwa kwenye kiti cha magurudumu kwa miaka sitini na sita, alitumikia miaka kumi na saba katika serikali ya Marekani kama—kama mbunge, na kadhalika, sikuwa nimewahi kumwona maishani mwangu. Naye Daktari Roy E. Davis wa Kanisa la Kimishenari la Baptisti ambaye alinibatiza katika imani ya Baptisti, ilikuwa ni, ama, tunaouita ushirika

wa Kibaptisti...Tunaamini ya kwamba, katika kanisa la Baptisti, ya kwamba Roho huwabatiza katika ule Mwili, bali sisi tunabatizwa...Kama umekuwa Mkampbeli, labda umezamishwa vyovyote utakavyo, kisha unaingia katika kanisa la Baptisti, huna budi kubatizwa katika ushirika huo. Kwa hiyo tunakuita kubatizwa katika ushirika wa kanisa la Baptisti.

¹⁸ Yeye ndiye, alimtuma Mbunge Upshaw kule aliyekuwa... naye alikuwa...Sikuwahi kumwona, niliingia tu jengoni kule Los Angeles, ambako maelfu mara maelfu kwenye viti vya magurudumu kila mahali, nami nikamwona katika ono, na kuanza kuzungumza, naye akaponywa usiku huo. Kwa mara ya kwanza kutoka kwenye kiti hicho, bila magongo hayo na kadhalika, kwa miaka sitini na sita, Mbunge William D. Upshaw. Rafiki msiri wa Churchill, na hao wote.

¹⁹ Na kama vile ninyi nyote mjuavyo kwamba nilipoenda kule na kumwomba Mfalme George alipokuwa na ugonjwa wa kushupaa mishipa, naye akaponywa mara moja, kesho yake akacheza mashimo kumi na manane ya gofu, na hata asingeweza kuketi kwa dakika chache tu kwa wakati mmoja.

²⁰ Nami nilikuwa huko kwa Gustaf. Na ndugu ya Gustaf ni Mpentekoste. Basi kwa nini ninyi, baadhi yenu watu mnauchezea Upentekoste? Ni kwa sababu mnaishi hapa katika mji mdogo, wala hamjui ulimwengu wote. Asilimia arobaini ya serikali yetu ni Wapentekoste, hiyo ni kweli, ama wana ushawishi wa Kipentekoste. Billy Graham alisema, "Huwezi tena kulificha kanisa la Kipentekoste, ndilo kanisa linalopanuka upesi kuliko yote ulimwenguni." *Mgeni Wetu Wa Jumapili*, kanisa Katoliki, lilitoa tamshi gani? kwamba mwaka jana pekee Wapentekoste walikuwa na waongofu milioni moja na laki tano waliosajiliwa, zaidi ya hayo mengine yote yakiwekwa pamoja. Sisi si lundo la takataka, tumetoka kwenye kichochoro, tuko juu utukufuni, ndivyo ilivyo, lakini, kanisa la Kipentekoste, na maafisa wa serikali, na kadhalika.

²¹ Nilikula kiamshakinywa pamoja na Bw. Nixon pale pale Washington, DC, kisha nikazungumza katika siku chache na baadhi ya maseneta ya jimbo nyumbani kwangu, hebu mwalize katibu wangu. Mahojiano haya ya faraghani, kama tuliyokuwa nayo asubuhi ya leo, na yale tuliyo nayo asubuhi ambapo watu wanakuja kuona yale Bwana anayosema, wanakaa pale, tunangojea pale mpaka Bwana atakaponena, si kama maono haya madogo mnayoona hapa, ninamaanisha, mnayafanya, bali madaktari, viongozi wa serikali, wabunge, watawala kutoka kote ulimwenguni.

²² Nilikuwa nikizungumza na katibu wangu. Huyu ni mama mkwe wa-...baba mkwe wake na mama mkwe wake wameketi papo hapo sasa. Hivi majuzi mimi...Wanangojea kwenye orodha kimataifa, zaidi ya mia sita wanaongojea sasa kutoka

kote ulimwenguni, wanaingia na kuketi mbele za Bwana, nasi tunaomba mpaka anashuka na kuwaambia la kufanya, madaktari, viongozi wa serikali, wanasheria, wabunge, na kadhalika kutoka nchini kote, hata nimekuwa na madaktari kutoka Kliniki ya Mayo Brothers. Si kitu cha uvumi tu, enyi marafiki: Mungu. Kwa hiyo, hivi ndivyo maono yalivyo.

²³ Sasa, katika mikutano hii, mikutano hii ya kiinjalisti, hamwoni moja kati ya kumi yake. Waulizeni ndugu wanaoambatana nami. Mnaona? Haya ni madogo tu... haya ni mambo unayofanya mwenyewe.

²⁴ Sasa, hapa, nami nitarudi kwenye hoja yangu, samahani kwa kuiacha. Lakini tunaenda kwenye kanivali, na kuna ninii kubwa mno, ama, sarakasi, kuna uzio mkubwa wa ubao kuizunguka, ha—hatujui jinsi ya kuuruka, kwa hiyo tunataka kuona kilichokuwa humo ndani.

²⁵ Wala hakuna mtu ulimwenguni ila yule anayetaka kujua alikotoka, kwamba yeye ni nani, na anakoelekea. Kuna Kitabu kimoja tu kinachoweza kukwambia, na hicho ni *Hiki*, kwamba, wewe ni nani, unatoka wapi, na unakoenda. Lakini kila mwanadamu anapenda kuangalia ng'ambo ya pazia kuona kilichoko upande huo mwingine, vema, tutafanya hivyo sasa, kwa ajili ya mfano.

²⁶ Na sasa, tunaenda zetu, nami ninamwangalia ndugu huyu, nami ni... mtu anayeonekana mwenye nguvu, mkubwa, mkakamavu, huku mimi, jamaa mdogo, mwembamba, vema, nafikiri labda anaweza kufanya sehemu yake kuingia kuona ma—ma—maonyesho, kilicho ndani. Vema, nitafanyaje hilo?

²⁷ Muda si muda mwajua, ilitokea nilichungulia shimo la kifundo, huko juu sana. Sasa, yeye hawezi kufikia huko juu, mnaona, ila ninaweza, kwa hiyo, bali kufanya hivyo, sina budi kunyosha mkono, na kuruka juu sana, kisha nishikilie tu kwa vidole vyangu, na kujivuta juu, ndipo nichungulie kwenye shimo hilo la fundo, nusura initoe pumzi, nami ninarudi chini.

“Uliona nini, Ndugu Branham?”

“Twiga.”

“Loo, kweli?”

“Uh-huh.”

“Uliona nini tena?”

“Huyo tu ndiye nilikuwa na wakati wa kumwona. Karibu iniue, mnaona.”

“Tazama uone kama unaweza kuona kitu kingine.”

²⁸ Sasa, hamtambui hilo, bali hilo ni wewe jukwaani, na hilo ni wewe umeketi huko nje, wewe ndiwe unayeondoa nguvu kutoka kwangu. Jana usiku, mtu fulani alikuwa anakuja,

karibu nianguke mara nne au tano nikitoka. Hamninii, watu hawatambui hilo. Laiti mngeliisoma Biblia!

²⁹ Hivi mnajua ya kwamba washairi, ama manabii, ama kadhalika, wanaingia katika uvuvio, wakati mwingine hata hawajui walipo? Je, uliwahi kusoma juu ya Stephen Foster? Aliandika *Maskani Ya Kale Ya Kentucky, Kushuka Mbali Sana Kwenye Mto Swanee*, aliipa Marekani nyimbo zake bora sana za jadi. Alihesabiwa kuwa mwenye fadhaa, kila wakati angeandika wimbo, uvuvio, kisha angetoka na kwenda kulewa. Wakati mmoja alipoandika, alitoka, alikuwa tu ametoka nje, naye akachukua wembe, akamwitwa mtumishi, kisha akajiua, akakata koo lake.

³⁰ Mliwahi kusikia kuhusu William Cowper? Bila shaka, mmesikia. Nilisimama kando ya kaburi lake, hivi majuzi, na kulia. Yeye—yeye alihesabiwa huko Uingereza ja—jamaa mjinga, mwendawazimu. Mtu yeyote ambaye ni wa kiroho kweli, sayansi inasema, yuko hatua moja tu kutoka kwenye kichaa, kutoka ulimwenguni. Kwa hiyo, ni akili ya mwanadamu ikijaribu kukabiliana na nia *hiyo* hapo, huwezi, hutambui, hakuna mtu atakayepata kujua, upande huu wa Umilele, inachomaanisha.

³¹ Kwa hiyo basi William Cowper, hatimaye ile siku... Mnakumbuka wakati alipojaribu hata kuingia kwenye teksu, aende akajiu? Akarudi, akachukua kamba, na akajaribu kujinyonga, ki—kisha akashuka, akajaribu kujizamisha mtoni, ndipo basi akaandika ule wimbo maarufu:

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini
ya hayo mafuriko,
Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

³² Hebu mwangalieni nabii Yona, mara alipotoka katika tumbo la nyangumi, kisha akaenda na kutoa unabii wake, maadamu tu yeye... uvuvio ulikuwa juu yake, akitoa unabii wake alikuwa sawa, lakini wakati uvuvio ulipomwacha, aliketi juu ya mlima na kumwomba Mungu ayachukue maisha yake.

³³ Nabii Eliya, chini ya o—ono la Bwana, alijiandaa na kuita Moto kutoka Mbinguni, akaagiza mvua kutoka mbinguni siku iyo hiyo, na kuwaua makuhani mia nne mwenyewe, ndipo basi, wakati uvuvio ulipomwacha, alilikimbia tisho la mwanamke, naye alikuwa siku arobaini mchana na usiku huko nyikani, bila hata kujua mahali alipokuwa, akizunguka—zunguka, ndipo Mungu akamkuta amejificha pangoni. Je, hilo ni la Kimaandiko?

³⁴ Mnaona, watu hawatambui hilo. Hamtambui jinsi haya... Unasema, “Vema, laiti ningalikuwa na huduma kama hiyo!” Ungetaka kuiondoa upesi sana. Hutambui kile inachokufanyia, inakuu. Lakini ni—ni... Mungu amekupa wewe.

³⁵ Wakosoaji hucheka, hudhihaki, na kila kitu, nami nikisimama papa hapa, ninajua kile wanachowazia. Hakika, ninaamini. Nilizoea kuwafichua, na kusema kila kitu, lakini nilipofanya hivyo, niliona inaumiza. Yesu alisema myaache yakue pamoja, msiyang'oe magugu, huo ni wakati wa Mungu mwishoni wa kuyang'oa magugu, mnaona, mwishoni mwa mavuno, yaacheni tu. Mnaona? Nasonga mbele tu, nina huduma ya kutekeleza, na, kwa hiyo, Mungu wa kumtumikia, nami nafanya tu vizuri niwezavyo, kisha naendelea mbele.

³⁶ Vema, sasa, unapokuja jukwaani, huyo ni wewe unayefanya hivyo, kama yule mwanamke aliyeligusa vazi Lake, imani yako mwenyewe ndiyo inayofanya hivyo, sina uhusiano wowote nayo. Kwangu mimi si—siwezi kufanya lo... Nimemwomba Mungu jambo fulani tena na tena, mimi mwenyewe, kwa miaka mitano iliyopita, wala hata hataniambia Neno juu yake. Mama yangu mwenyewe alikuwa amelala hapa mahututi, na kusema, “Mwanangu, mwisho wangu utakuwa nini?” Huku maskini mama yangu mpendwa, nisingeweza kumwambia mpaka Mungu aniambie. Mnaona? Mimi... Yeye hana budi kunena, mimi sineni, ni Yeye. Wala si mimi ninayesababisha ono hapa jukwaani.

³⁷ Waulizeni ndugu zangu walio pamoja nami, juma hili sijakula kitu ila biskuti na maziwa, hiyo ni kweli. Kufunga tu, kungojea, kuona ni njia gani Roho ataniongoza. Wale wavulana mlangoni walisema, “Kuna mlo mkubwa mtamu sana hapa chini. Ndugu Branham, jinsi unavyopenda, uh, kwenda kwenye ninii-...!”

³⁸ Nikasema, “Ninapenda, bali si katika ibada za uponyaji.” Unamngojea Bwana. Hii huja tu kwa kufunga na kuomba. Hii hapa kesho usiku inakuja wakati viwete, na wagonjwa hospitalini, na watu mahututi watakuwa wameketi hapa, kujiandaa kwa ajili yake. Kama unawapenda watu... Na kama huwapendi watu, afadhali uondoke hudumani, hivyo tu, kwa sababu, basi, endapo moyo wako hauwaki kwa ajili yao! Afadhali ungesema jambo zuri kumhusu mwanangu kuliko ungesema kunihusu mimi, kwa sababu huyo ni mwanangu.

³⁹ Na ikiwa hatuwezi kupendana, tutampendaje Mungu ambaye hatujamwona? Mnaona? Hatuna budi kupata *kitu* hicho, hatuna budi kupendana, ingawa tunatofautiana, hamna budi kupenda kwa vyovyote vile. Huwezi kulidanganyia, huna budi kufanya hivyo kweli. Huna budi... Na hiyo... Nguvu kuu kuliko zote nilizowahi kuona katika uponyaji ni upendo, wakati unapokuwa na huruma na upendo kwa watu, ukijaribu kuwasaidia.

⁴⁰ Wakati mwingine mimi huwakemea ki—kisha narudi nyumbani, nawazia tu, “Bwana, nilifanya hivyo kwa sababu gani?” Lakini ni kwa sababu ninawapenda. Kama itanibidi

kumkemea mvulana wangu mdogo kwa kukimbia barabarani, atauawa nisipomwondoa kwenye barabara hiyo, wakati mwingine inanibidi kumpiga mijeledi, kumsahihisha, kusema, “Mwanangu, kaa mbali na barabara hiyo,” si kwa sababu simpendi mtoto huyo, ni kwa sababu *ninampenda*. Hivyo ndivyo Mungu anavyopaswa kutufanyia, kutukemea, na kututikisa, kutufanya nanii wa kweli... Mtu anayemwacha mtoto wake afanye chochote si mzazi mwema. Hiyo ni kweli. Kuna mengi sana ya hayo Marekani siku hizi, naam bwana, tunahitaji akina mama wa mtindo wa kale.

⁴¹ Sasa, mtu fulani anakuja jukwaani, mama. Mimi hapa, nimejistarehesha. Naye anakuja, yeye ni nani? Sijawahi kumwona, simjui. Yeye ni nani? Sijui. “Ee Mungu, ninakutegemea Wewe sasa. Siku nzima niliomba. Ni kitu gani, Bwana?”

“Piga hatua kwenye Biblia hii, hapa.”

⁴² “Mungu, hilo hapo Neno Lako, Wewe ulitoa ahadi, kati yangu na mwanamke huyo linasimama Neno Lako. Roho Wako yuko hapa mahali fulani. Mungu, labda jambo moja ambalo huenda likaliwasha moto jengo hili lote. Labda Roho Mtakatifu ameingia, akaondoa kutokuamini kwote, usiku wa leo. Hakuna kitu hapa ndani, ila kile kitakachoniamini, kila kitu kitaamini, kwa sababu nimelihubiri kwa urahisi tu niwezavyo, nao wamesoma Biblia, wanajua ni kweli, na ni ahadi kwa ajili ya siku hii. Hakika, watafanya hivyo, Bwana.”

⁴³ Kisha nikijaribu kujistarehesha, nikizungumza. Muda si muda mwajua, ninafanya nini? Ninapanda juu, ninapanda juu, kuona ni aina gani ya imani ambayo mwanamke huyo anayo, hatimaye, ninakuta ana imani. Inafanya nini? Inagusa. Ndipo kati yangu na yeye, ninaiona. Sasa, nitaenda wapi? Hapa, juu, juu, juu, nainyakua, “Una uvimbe.”

“Naam, bwana.”

⁴⁴ Unaligeukia kusanyiko, “Alibahatisha hilo.” Mnaona? “Vema, hiyo ni telepathia ya kiakili. Dk. Jones alisema ilikuwa *hivi-na-hivi*. Loo, huko ni kusoma mawazo.” Mnaona, wewe hapo tena.

⁴⁵ Vema, unaweza kusema nini? Unaangalia huko nje, hapa ameketi *huyu, yule, hapa* juu, chini, hiyo hapo imerudi *hapa, hapa*, “Mungu, nifanyeje...? Vema, Bwana, ilikubidi kupitia jambo lile lile.”

⁴⁶ Sasa, ni kitu gani tena kilikuwa...? Ana shida gani tena? Wewe hapa unaenda tena. Wewe tayari, vidole vinauma tuseme, vikining’inia hapo, sasa moyo wako unauma. Unaona? Kisha unapanda juu tena, “Na isitoshe, una TB, ulikuwa kwa daktari hivi majuzi, naye akakwambia, ulikuwa... A—alikuwa ni mtu mrefu. *Whiu!*”

“Alisoma mawazo yao.” Si ajabu hiyo?

Hata Wakristo wakisema, “Vema, nadhani ni sawa.” Mnaona?

⁴⁷ Vema, baada ya kitambo kidogo, huyo anapita. Huyu hapa mwingine. Basi karibu umenyong’onyea kabisa. Unaona? Huyu hapa mwingine. Vema, huo hapo mlolongo mzima wao wamesimama, usipomfikia kila mmoja wao, jamani, wao “sikuombewa kamwe, kuna kasoro.”

⁴⁸ Mnaona—mnaona ninajaribu kutumia karama ya kinabii katika ibada ya kiinjilisti, hiyo ndiyo sababu haifanyi kazi vizuri sana. Inafanya kazi Afrika, inafanya mahali pengine popote ila Marekani, pengine popote ila hapa, itafanya kazi, haifanyi kazi hapa. Watu kabisa hawalipati, sijui ni kwa nini, bali hawalipati.

⁴⁹ Jambo hilo moja linaweza kutokea Afrika, maelfu watakimbia madhabahuni, wakipiga mayowe, wakilia, wakiruka kutoka kwenye viti vyao vya magurudumu, kama itawabidi kutambaa, ama chochote kile, wanamwamini Mungu, hivyo tu, wanalipata. Lakini tumekuwa, mnaona, tumeshindiliwa *itikadi* nyingi sana mbalimbali na mambo mengi sana mbalimbali, mtu mmoja anasema ni *hivi*, mtu fulani anasema ni *vile*, “Yeye ni mfuasi wa kanisa lingine, yeye si—yeye si mmoja wetu. Yeye ni mtakatifu anayejifingirisha. Hu—hu—huenda akawa ni kijumbe, huenda akawa ni ibilisi.” Mnaona, na hayo yote ambayo yanahuzunisha tu nanii. . . Halafu mtu fulani asema, “Ha, nitatoka hapa sasa hivi.” Loo! Mnaona?

⁵⁰ Sasa, unawezaje kufanya mkutano chini ya hayo? Hebu niwaulizeni jambo fulani. Hebu litupe kusanyiko hili kwa nia moja, kwa imani moja wakati mmoja, hebu niwageukieni, katika Jina la Bwana, hakutakuwako na kiti cha magurudumu hata kimoja kitakachosalia hapa ndani, bali watu watakuwa wakitembea. Hebu lijaribu tu wakati mmoja, uone. Nimeliona, elfu ishirini na tano waliupata, viti vya magurudumu, machela, na kadhalika, na wakatembea.

⁵¹ Lakini huna budi kuhudumu, kwa vyovyote vile. Hili ndilo taifa lililo na pesa za kunituma kule, hao hawana pesa za kunileta. Sina msaada wowote mkubwa, jambo pekee linalonilazimu kufanya ni kumtegemea Mungu tu, “U—Unirehemu, fanya jambo fulani. Popote uniongozapo nitaenda.” Na hivyo ndivyo ninavyofanya. Mnaona?

⁵² Sasa, pengine, labda kiongozi wa hiyo sarakasi anakuja sasa, “Kwani ninyi wavulana mnaangalia nini?”

“Tulikuwa tukiangalia ndani, bwana.”

⁵³ “Loo, vema, njoni hapa.” Yeye ni jamaa mkubwa mno, anainama, ananibeba kwa mkono wake, kasema, “Nitakwambia jinsi hii inavyoedelea, Ndugu Branham. Unaona maonyesho yale *pale*?”

“Naam.”

⁵⁴ “Sasa, hapo ndipo safari ya Garland inapoanzia, *pale*. Wanakuja hapa wanazunguka *hivi*, wanapitia *hapa*, kisha wanafanya *hivi*. Nayo *hii* inafanya *hivi*, na *hii*, *vile*.”

“Loo, naam, bwana,” nimeketi kwenye kiganja cha mkono wake.

“Na *hii* ni *hii*, na *hii* ndiyo.” Ananiweka chini pale kwenye lile jukwaa maalum, mwajua, naye akanionyesha kila kitu kilichokuwa kinaenda kutukia.

“Loo, kumbe. Asante, bwana. Asante sana.”

“Sasa, uwe mvulana mzuri.”

“Asante, bwana.”

“Nini kilitukia? Uliona nini?”

⁵⁵ “Loo, Mungu asifiwe!” Mnaona, mnaona, sijachoka. Mnaona? Aliniinua tu na kunionyesha. Sasa, hiyo ni *wewe* ukitumia karama ya Mungu, ama Mungu akitumia karama Yake Mwenyewe. Mnaona?

Sasa, unasema, “Hilo ni la Kimaandiko?” Naam, ndugu.

⁵⁶ Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake wakati mmoja, Naye akasema, “Nimekuwa dhafu.” Hiyo ni kweli? Lakini siku moja, wakati alipokuwa katika nyumba ya Martha, na Mariamu, na hao wengine, Yeye...ninii...Mungu alimwonyesha, Alisema hakutenda neno mpaka Baba alipomwonyesha, ndipo Mungu akamwonyesha ya kwamba Lazaro atakufa. Kwa hiyo, Yeye akasema, “Wewe nenda zako, nao wataagizia uitwe.” Sasa, nitathibitisha jambo hilo. Akasema, “Ondoka, na baada ya siku nne atakufa. Kisha urudi, utamwamsha, uende kaburini ukamwamshe,” na kadhalika. Kwa sababu ilimbidi kufanya hivyo, ama kama hakufanya hivyo, alisema uongo.

⁵⁷ Kwa hiyo akaenda, nao wakaagizia aitwe. Je, alirudi? “Rafiki yako Lazaro ni mgonjwa, karibu kufa.” Alijua kile Baba alichokuwa amemwambia, kwa hiyo akaendelea mbele tu. Wakatuma mtu tena, “Lazaro ni mgonjwa. Njoo, mwone upesi sana, atakufa.” Akaendelea mbele tu.

⁵⁸ Kama ungaliagizia mchungaji wako aitwe, wala hakuja, ungalienda na kujiunga na kanisa lingine. Unaona? Hiyo ndiyo sababu hamfiki popote. Huna budi kumwamini mtumishi uliyetumiwa na Mungu. Unaona? Iwapo Yeye anaongozwa na Roho, mwacheni.

⁵⁹ Ndipo baada ya siku nne, Yesu akageuka, maana hivyo ndivyo Baba, bila shaka, alivyokuwa amemwambia, maana Yeye alisema hakufanya lolote mpaka Baba alipomwonyesha. Akageuka, akawaambia wanafunzi Wake, Yeye alijua wakati ulikuwa umetimia, akasema, “Rafiki yetu Lazaro amelala.”

“Loo,” wakasema, “anafanya vema.”

⁶⁰ Akasema, kisha akawaambia katika lugha yao wenyewe, kasema, “Amekufa. Na kwa ajili yenu, nina furaha sikuwako,” kwa hiyo, Yeye akasema, “lakini ninaenda kumwamsha.”

⁶¹ Ndipo alipofika kaburini, sikilizeni yale aliyosema, “Nakushukuru, Baba, Wewe *tayari* umenisikia,” mnaona, “umenisikia Mimi, lakini ninasema tu haya, hili, kwa ajili ya wale waliosimama karibu, nililisema kwa ajili yao.” Mnaona? Ndipo akasema, “Lazaro, njoo huku.” Lazaro akatoka.

⁶² Kamwe hakusema lolote kuhusu kuwa dhaifu, sivyo? Hiyo ilikuwa ni Mungu akitumia karama Yake, hiyo nyingine ilikuwa ni mwanamke akitumia karama Yake. Mnaona tofauti yake? Mnaelewa sasa? Mnaona, hivyo ndivyo ilivyo, ni wewe unayefanya hilo.

⁶³ Sasa, katika mahojiano, na kadhalika, wana nyakati ambapo Roho Mtakatifu, kama vile nikiketi asubuhi ya leo mbele ya mume na mke vijana, jinsi alivyopitia maishani mwao, anayachukua na kuyarudisha.

⁶⁴ Na, jamani, hapa daktari maarufu aliketi chumbani hivi majuzi, naye akaniuliza kuhusu jambo fulani. Nikasema, “Je, utaomba pamoja nami?”

Akasema, “Nitafanya hivyo, bwana.”

⁶⁵ Tukapiga magoti, tukaomba. Nikasema, “Sasa, unatafiti kuhusu kujenga kliniki. Na kuna jambo fulani linalokaribia kutukia. Nawe uliangalia mahali fulani pa kujenga kliniki hii, ulisema wasingeweza kupagusa kwa muda wa miaka ishirini na mitano, lakini,” nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, Daktari!”

Akasema, “Unafikiri huu mji unahitaji kliniki?”

Nikasema, “Naam, bwana, unahitaji kliniki. Nafikiri wewe ni daktari mzuri, kwa hiyo wewe nenda, na . . .”

Akasema, “Haiwezekani hata hivyo, haiwezi kuwako.” Kasema, “Tayari nimeshindania hilo mahakamani,” kasema, “huwezi kuijenga hapo.”

⁶⁶ Nikasema, “Itajengwa kwa tofali jekundu, itakuwa na paa jepesi juu yake, na karibu itakuwa urefu wa bloku ya mji, nayo itakuwa hapo, na jina lako litakuwa mbele yake, niliiona, BWANA ASEMA HIVI.”

Akasema, “Ningetaka kuamini hilo, bwana.”

⁶⁷ Nikasema, “Unakumbuka wakati uliponitumia mtu yule si muda mrefu uliopita ambaye hata hakuwa na ini, nusu yake limeliwa, yule mhudumu? Asubuhi hiyo niliona hayo matofaa matano yakishuka, ndipo tofaa kubwa lenye afya likayala hayo matofaa yasiyo na afya, nami nikakwambia BWANA ASEMA HIVI, ataishi, nawe ukasema, ‘Anawezaje kuishi bila ini ndani yake?’” Nikasema, “Yeye anahubiri, naye alichukua mahali

pangu kwenye Kanisa la Kibatisti la Milltown.” Nikasema, “Angali yuko.”

Akasema, “Loo, ninamkumbuka Kasisi William Hall, Kanisa la Kibatisti la Milltown.”

Nikasema, “Yeye angali yuko, hiyo imekuwa kama miaka mitano iliyopita.” Nikasema, “Kliniki yako itakuwepo.”

Akasema, “Natumaini unasema kweli.”

Nami nikasema, “Ati *unatumaini*?” Nikasema, “Yeye daima husema kweli.”

Na kwa hiyo kesho yake asubuhi akanipigia simu, akasema, “Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam?”

Akasema, “Ninaganda karibu kufa.” Na ilikuwa Julai.

Nikasema, “Ati unaganda karibu kufa?”

⁶⁸ Akasema, “Nimejaa mitetemo.” Kasema, “Walikuwa na mkutano huko Boston jana usiku pamoja na zabuni zote za mahali hapo, wakanichagua. Haitahitaji kungojea miaka ishirini na mitano, tayari imekwisha, tayari nimepanunua mahali hapo asubuhi ya leo.” Hiyo hapo kliniki, papo hapo usiku wa leo.

⁶⁹ Huko St. Louis, hivi majuzi tu, katika mkutano mkubwa wa matibabu alitoa hotuba, naye akasimulia hayo. Ina jina lake linalotokeza mlangoni mwake limechongwa kwa shaba. Akasema, “Mtu akishuku, daktari yeyote, mwambie anipigie simu nitailipia.” Um-hum. Jambo ndilo hilo. Loo, mnaona, marafiki, si chochote. . . Jambo ni kwamba, hamwezi kujiamsha, hivyo tu, hamwezi kujiamsha mpate uhalisi wa mambo yalivyo.

⁷⁰ Ninyi watoto, nanyi watu humu ndani katika viti vya magurudumu, mna jua kama ningeweza kuwasaidia, ningekuja kufanya hivyo, mwajua hilo. Uh-huh. Mungu aubariki moyo wako, bila shaka ningefanya hivyo. Lakini ninyi si zaidi. . . Kumponya mtu aliye kwenye kiti cha magurudumu si zaidi ya kumponya mwenye ugonjwa wa moyo. Basi jambo kuu sana alilopata kufanya lilikuwa ni kuokoa nafsi ya mwanadamu, kubadilisha mwelekeo wake wote, na kila kitu. Kwa kuwa unafiki tu umefungwa milele, hujafungwa, la, bwana. Nimeona makumi ya maelfu ya viti vya magurudumu, ya watu wakiponywa wakatoka kwake, mnaona, nami najua.

⁷¹ Na ni kweli, mtu fulani alisema ya kwamba sarufi yangu ni mbovu. Ninakumbuka huko Fort Wayne, si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikihubiri huko B.E. Rediger, ambako binti yake alikuwa ameponywa wazimu siku chache zilizopita. Loo, mimi huyo tena, mambo mengi sana ya kusema. Msichana mwendawazimu aliyekuwa akienda kwenye chumba cha maiti. Nayo hiyo shule ya Katoliki hata isingeniruhusu kuingia, niliingia kama mgeni, nikazungumza na huyo msichana

dakika chache. Nikasema, nikamwambia baba yake (nilikuwa nikiambatana na mama wa huyo msichana.), nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, yuna akili timamu.”

Mama yake akanishika kiunoni, naye akasema, akamwangalia mumewe, akasema, “Kamwe hakosei.”

Nikasema, “Sasa, yeye hakumaanisha mimi, alimaanisha Roho wa Bwana.”

⁷² Na yapata saa mbili baadaye, baba alinipigia simu, akilia, akasema, “Ndugu Branham, sijui la kusema.” Binti yake alikuwa tu na umri wa miaka kumi na minane, mwalimu katika muziki, na kucheza lele, na kadhalika, masomo yale yale ambayo binti yangu anasomea. Akasema, “Sijui la kusema.” Kasema, “Msichana huyo alijirudia mara moja, nao madaktari hawa wanashauriana sasa hivi.” Kasema, “Anaenda nyumbani pamoja nasi alasiri ya leo.” Kweli. Mnaona? Hiyo ni kweli. Nikasema . . . Akasema, “Loo, nitalitangaza kote nchini!”

Nikasema, “Shh, usimwambie mtu yeyote. Endelea, mshukuru Mungu tu, kisha uendelee, unaona. Endelea mbele tu.” Yeye ni wa ajabu kama tu utamwamini.

⁷³ Maskini jambo moja zaidi kwenu ninyi watu: Kwa sababu tu kwamba ati uko hapa mkutanoni, na unakubali uponyaji wako, hautendeki mara moja, usijali hilo, litatendeka kama una imani ya kutosha kuamini litatendeka.

⁷⁴ Kulikuwa na mwanamke aliyekuja mkutanoni usiku mmoja, akapitia, alikuwa na ugonjwa wa tumbo. Roho Mtakatifu akamwambia, “Wewe ni Bibi *Nanii*, ulitoka mahali fulani.” Kasema, “Una ugonjwa wa tumbo.” Kisha kasema, “Jambo ni kwamba, ni kidonda cha duodeni.” Kasema, “Ni hatari sana, na daktari anasema huenda ukatokwa na damu kwake wakati mwingine, kwa sababu amekuwa akitaka kukufanyia upasuaji.” Nikasema, “Lakini unaogopa upasuaji, na kwa hiyo, ni vigumu kwako kula chochote kamwe, ila michuzi tu, na mbalimbali tu, kama mchuzi wa nyama, na kadhalika.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.” Naye akasema, “Je, anasema kweli, Bw. Branham?”

⁷⁵ Nikasema, “Bila shaka, daktari wako anasema kweli.” Nami nikasema, “Sababu yake, ni kwa kuwa ilisababishwa na fadhaa, uko na fadhaa wakati wote.”

Akasema, “Nilikuwa mtoto mwenye wasiwasi.”

⁷⁶ Nikamwangalia, nami nikamwona ameketi karibu na mnofu mzuri, mkubwa, akila, mwajua, na kula kipande cha sambusa ya tofaa, hicho ndicho nilichoona katika ono, nikasema, “Lakini BWANA ASEMA HIVI!”

⁷⁷ Angalini asemayo. Mnaona? Wewe ndiwe unayemfanya aseme *hili*, bali ni kuangalia kile anachosema nyuma yake, jambo ndilo hilo, mnaona. Unasema, “Una kansa,” nawe unajua

hilo, lakini angalia kile Yeye asemacho kuhusu kansa hiyo, unaona, hapo ndipo unapoliangalia. Kwa hiyo basi—basi... Yeye... Naye akamwambia.

Kwa hiyo akasema, “Ninatoka kwenda kula.” Kwa hiyo akatoka akaenda, akala.

⁷⁸ Na ki—kidogo nyuma ya huyo akaja mama aliyekuwa na uvimbe mkubwa kwenye koo lake. Ndipo Roho Mtakatifu akamwambia, “Uvimbe huo utakuacha, BWANA ASEMA HIVI.”

⁷⁹ Kwa hiyo ilitokea kwamba walikuwa wanawake majirani. Na kwa hiyo, kesho yake akajaribu kula, na loo, jamani, nusura afe. Na kwa hiyo, akajaribu kwa siku mbili ama tatu, naye angetapika tu, na kugooka, na damu kuruka kutoka kinywani mwake, na kadhalika. Naye, baada ya yapata juma moja, mumewe, akiwa ni Mkristo, lakini akasema, “Mpenzi,” kasema, “unaleta aibu juu ya huduma.” Kasema, “Haikupasi kusema mambo kama hayo.”

⁸⁰ Akaanza kulia, akasema, “Mume wangu, sikiliza,” akasema, “mtu huyo kamwe hakuniona maishani mwake, na kwa Nguvu za namna fulani ambazo ninaamini zilikuwa ni Roho Mtakatifu, kulingana na yale ninayosoma katika Biblia hii, aliniambia shida yangu ilikuwa ni nini, nilikuwa ni nani, kikamilifu kabisa, kisha akaniambia kwamba BWANA ASEMA HIVI ya kwamba nitakuwa mzima.” Akasema, “Mpaka wakati huo utakapokuja, nitakuwa nikifanya hivyo.” Vema. Vema.

⁸¹ Kwa hiyo, akasema, “Endelea, kipasue kidonda chako, ndipo utatokwa na damu hata ufe.” Akaendelea mbele tu. Bila shaka yeye—yeye hakuwa na... Mnaona, halikutendeka kwake, lilitendeka kwa mkewe, haikuwa imani yake, ilikuwa ni ya mkewe.

⁸² Vema, karibu miezi miwili ikapita, hakuna kilichotukia. Asubuhi moja watoto walikuwa wameondoka, wameenda shuleni, naye alikuwa akiosha vyombo, na alikuwa anaimba, ndipo baada ya kitambo kidogo, akashikwa na hisia ya ajabu sana, akasema. Alikuwa akashuhudia hilo. Kwa hiyo, akasema hisia ya ajabu sana ilipitia juu yake, mara akashikwa na njaa sana, akasema. Vema, watoto waliacha shayiri kwenye sahani zao, mwajua, nadhani kina mama hufanya hivyo, na kwa hiyo akachukua sha—shayiri kidogo, na kuila, naye akawazia, yeye, kwa kawaida, angetapika. Kwa hiyo, akachukua shayiri kidogo, naye akaila, nayo tosti hiyo ilionekana nzuri sana, alikuwa akila tosti baadhi ya watoto walikuwa wameacha.

⁸³ Kwa hiyo akaendelea kwa dakika chache, naye alikuwa angali ana njaa, hakutapika, kwa hiyo akajichotea tu kidogo, akazikoroga, akala kipande cha tosti, akaendelea kuosha, alijisikia tu vizuri akiifanyia usafi nyumba yake. Akashikwa na njaa sana tena, kwa hiyo akaenda tu na kujikaangia mayai mawili, na nyama kidogo ya nguruwe, akanywa kikombe cha

kahawa, ndipo akawa na yubile ya ulaji bora, kwa hiyo akajiandaa kabisa kwa ajili yake. Na kwa hiyo, alikula tu chote alichoweza, akangojea, mpaka yapata saa nne, hakuna kitu kilichotukia, akashikwa na njaa tena, kwa hiyo akawaza, “Loo, Mungu asifiwe!” Akasema, “Nitashuka kwenda, nikamwambie jirani yangu.”

⁸⁴ Basi alipofika kule chini, alimsikia mtu fulani akipiga mayowe na kulia, kwa hiyo akakimbia mlangoni na kuutikisa mlango, wala hakuna mtu aliyejibu, akadhani labda mtu fulani amekufa. Na kwa hiyo, akaingia nyumbani upesi sana, na hapa mwanamke huyu ameshika shuka mkononi mwake, akiitikisa namna *hiyo*, na kupiga mayowe, kwa sauti yake yote. Naye akasema, “Kwani kuna nini?”

⁸⁵ Akasema, “Unajua nini?” Kasema, “Jana usiku nilikuwa nimesimama mbele ya kioo, nikiangalia lile fundo shingoni mwangu, sasa angalia, limetoweka.” Kasema, “Nimetikisa kila shuka, kila kitu kingine, nikijaribu niwezavyo kulipata. Nilipoamka asubuhi ya leo, na . . .”

⁸⁶ Sasa, ninayo majina yao na anwani, mnaona, taarifa zilizoandikwa. Basi mnaona, ilivyokuwa, wakati yule Malaika wa Mungu. . . Sasa, mtu yeyote ambaye ni mwanafunzi wa Biblia anajua kwamba wakati mwingine Mungu hajitokezi moja kwa moja jukwaani wakati Yeye—wakati Yeye anapapaswa kuja, ambapo tunafikiri anapaswa kuja. Mnakumbuka, Danieli aliomba, ilikuwa siku ishirini na moja kabla Malaika hajaweza kumfikia. Hiyo ni kweli? Vema, ni wangapi wanaojua hilo?

⁸⁷ Nini kilitukia? Malaika yule yule wa Mungu aliyetoa ahadi, sio mimi sasa, sikuwa na uhusiano wowote nalo, sikuwajua, bali nilisema, “BWANA ASEMA HIVI,” ilimchukua karibu miezi miwili, bali alikuwa akipitia kwenye ujirani akithibitisha Neno hilo alilokuwa amenena. Utukufu kwa Mungu! Kama huyo si Mungu yeye yule wa Biblia, siujui Biblia yangu. Kweli kabisa. Hilo limetukia mara makumi ya mamia, ewe rafiki.

⁸⁸ Kwa hiyo, ninasema hivyo kwa sababu gani? Kuijenga imani yenu kwa ajili ya ibada ya uponyaji kesho usiku. Ninawatakeni mnini. . . kama ni. . . Sasa, msilidanganyie. Halitadanganya, huwezi kumdanganya ibilisi. Mnakumbuka wakati Yesu alipolipa kanisa Lake, kama, Yeye alipolipa kanisa Lake nguvu katika Mathayo Mtakatifu mlango wa 10 kutoa pepo, kuponya wagonjwa, na—na wenye ukoma, na kufufua wafu, hiyo ni kweli? Sasa, ninataka mtu ambaye haamini katika uponyaji wa Kiungu, anionyeshe, kwa Maandiko, ambapo Yeye aliwahi kuziondoa nguvu hizo kanisani. Ninataka sura, Kitabu, na kifungu. Ambapo alilipa Kanisa Lake nguvu hizo, ninaweza kuwaonyesha sura, Kitabu, na kifungu, ambapo aliwaambia zingekuwa kwa jamii zote, mahali pote, ulimwenguni kote. Sasa, hebu niambieni mahali aliposema, “Nilikosea, sina budi

kulighairi.” Hebu mnionyeshe hilo, mkosoaji fulani. Haliko katika Neno la Mungu.

⁸⁹ Sasa, mnaona, si...Mahali unapoangalia, rafiki yangu mkosoaji, ni hapa: unaangalia ule udhaifu, unaangalia kile watu wanachofanya juu yake, lakini usiangalie hicho, angalia kile Mungu alichosema kulihusu. Unaona? Jambo ndilo hilo. Unaangalia kwingineko, una makengeza. Unaona? Naye mtu mwenye makengeza hajui anakoelekea. Unaona? Kwa hiyo unaninii tu, unamwangalia Mungu kwa jicho moja, yale Mungu aliyosema, si yale watu wanayofanya kulihusu, yale seminari iliyosema, bali yale Mungu aliyosema. Na kama *Hili* silo Neno la Mungu, basi nenda kachukue kitu ambacho ni Neno la Mungu.

⁹⁰ Si ajabu inabidi kasisi, inabidi kasisi wa Katoliki kuwa mwerevu sana, ana vitabu mia sita anavyopaswa kujifunza ambavyo ni vitakatifu tu kwake kama hiyo Biblia, Biblia zingine mia sita, kama, za watu wengine walioandika vitabu ambavyo hana budi kuvisoma. Mwerevu, hakuna njia ya kuendana nao, kuzungumzia, inapofikia mambo ya kiakili, bali Mungu hatumii hiyo hata kidogo, huo ni upumbavu Kwake. Unyenyekevu wa kumwamini Yesu Kristo ndio Mungu anaoheshimu. Hulifanya hata mpumbavu asikosee humo.

⁹¹ Sasa, sasa, angalieni hapa, ninii... Yesu katika Mathayo 10, alikuwa amewapa nguvu za kuwaponya wagonjwa. Wakatoka, wakawatoa pepo, wakarudi wakishangilia, na kadhalika. Ndipo siku kumi baada ya wakati huo, walishindwa kabisa na ugonjwa wa kifafa. Hiyo ni kweli. Ninaweza kuwazia nikimsikia Andrea akisema, “Rudini nyuma, enyi wavulana.”

“Hakika hamwezi kufanya hivyo.”

⁹² “Hebu niwaonyeshe jinsi nilivyofanya huko Kapernaumu: Njoni hapa! *Grrr!* BWANA ASEMA HIVI, toka kwake, ewe ibilisi! Toka ndani yake, ewe ibilisi! Haleluya! Toka ndani yake, ewe ibilisi!” Mvulana aliendelea tu na kifafa.

⁹³ Nami ninaweza kumsikia Petro akisema, “Loo, kumbukeni, ninyi nyote hamjui. Hebu niwaonyeshe jinsi nilivyofanya huko Yafa. Njoo hapa, hebu nimchukue.” Anamvuta kule, kasema, “Hivi ndivyo unavyofanya!” Wote walishindwa, si kwa sababu hawakuwa na nguvu.

⁹⁴ Sasa, angalieni, na baada ya kitambo kidogo, angalieni, akishuka kutoka mlimani kule, ninamwona akija, akitembea kwa utulivu. Biblia ilisema hakuna uzuri hata tumtamani, labda Jamaa mdogo, aliyeinama mabega, lakini alipokuja akitembea mahali alipokuwa, ambapo wao...baba huyo alikimbia na kusema, “Bwana, nilimleta mwanangu kwa wanafunzi Wako, bali wasingeweza kumfanyia chochote.” Akasema, “Utatusaidia?”

Naye akasema, “Ninaweza kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio.” Mnaona?

Akasema, “Bwana, naamini; saidia kutokuamini kwangu.”

⁹⁵ Ndugu, wakati huyo ibilisi alipotembea mbele Zake, alijua alikutana naye katika kiwango tofauti na kile hao wanafunzi walikuwa nacho.

Kasema, “Toka ndani yake.”

Ndipo mvulana huyo akaanguka, na kupata kifafa kibaya sana alichowahi kuwa nacho, kisha akanyooka, akakakamaa. Wakasema, “Amekufa.”

“Hajafa. Mwinueni juu.”

⁹⁶ Wanafunzi wakaja, na kusema, sasa, sikilizeni, haya hapa mambo ya kisasa, “Vema, Bwana, nakisia uliondoa nguvu zetu zote kwetu, Kanisa halina nguvu tena.”

“La.”

“Kwa hiyo kwa nini tusingeweza kumtoa?”

Kasema, “Kwa sababu ya kutokuamini kwenu.” Hiyo ni kweli?

⁹⁷ Kanisa lingali lina nguvu, ninyi Wamethodisti hapa, mna nguvu hizo, ninyi Wabaptisti, Wapresbiteri, Wanazarayo, Pilgrim Holiness, bali mnaogopa kuzitumia. Hivyo tu. Ingenifaa nini kuwa na bunduki nzuri ya kuwindia, na kuiweka ukutani, naogopa kuitumia? Nisingeweza kupata mnyama yeyote, nina hakika. Vema, huenda nikachokora-chokora kabisa, na kupata milipuko kadhaa ya mapema, na nisitie risasi vizuri sana kwa mkono, Ndugu Gene, lakini ninapiga risasi kwa vyovyote vile, hivyo tu. Ninajaribu sana. Naam, bwana, kwa hiyo mtafanya hivyo. Hebu na tuamini, na tujue hilo kama tunaamini! Amina.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

⁹⁸ Bwana Yesu, wakati mwingine tunazungumza kama watoto, nasi tunafurahi kuwa hivyo, kwa kuwa kama tunajua mengi sana Wewe huwezi kutuongoza tena, lakini maadamu sisi ni watoto Wewe unatusamehe ujinga wetu, na—nasi tunautumainia tu mkono Wako. Wakati mwingine tunapiga mayowe, na kupiga makelele, na kufanya yasiyofaa, kwa sababu, Baba, sisi ni watoto, ha—ha—hatutegemei uwezo wetu wenyewe, tuna furaha tu kwamba tunaninii. . . tunaye Baba anayetulinda. Tuna furaha sana kwa ajili ya jambo hili.

⁹⁹ Bwana, kuna watu hapa ambao ni wagonjwa, wanaoteseka, baadhi yao wameokoka, wengine hawajaokoka, wengine wanaamini wameokoka wala hawajaokoka, wengine wameokoka, wao—wao ni wa kila namna tu, Baba, wote wamechanganyikana. Waweza kutusaidia usiku wa leo, tupate kuwa na uponyaji mmoja mkuu mno, wa hadhara kesho? Tujalie, Bwana. Jalia kuwe na kumwagwa kukuu sana kwa Roho Wako, Bwana, ninaomba ya kwamba utalijalia hivi kwamba, hata

hapatakuwa na mtu mnyonge atakayesalia humu jengoni. Tujalie, Bwana.

¹⁰⁰ Sasa, tutafungua kurasa za Neno. Sasa, siwezi kukifungua Kitabu hiki, ama hakuna mtu anayeweza, kimwili tu kwa mikono yangu, jalia Roho Mtakatifu akifungue na kutufasiria Maneno machache ambayo yangeijenga imani yetu hivi kwamba, kwamba kutokuamini kwote kutatuondokea, na kwamba tungeridhika kikamilifu na imani safi, isiyoghoshiwa katika Mungu ya kwamba Yeye huwaponya wagonjwa, huwaokoa waliopotea. Na kama kuna dhambi yoyote miongoni mwetu, Bwana, iondoe, tafadhali, Bwana. Na jalie tujitakase, usiku wa leo, kwa imani katika Damu ya Mwanao, Yesu Kristo, Bwana wetu. Tunaomba, katika Jina Lake, Amina.

¹⁰¹ Sasa, hapa nikiwazungumzia tu, na ni wakati wa kufunga. Nina Maandiko mengi kiasi ambayo nimeandika hapa ningetaka kuyarejea, huenda nisifikie lolote la hayo. Lakini kwa njia ya muktadha, sasa, sitachukua muda mrefu sana, kweli, natumaini sitakuchukua, bali ninaninii tu, ninataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Yeremia, mlango wa 8, kifungu cha 22. Hili ni swali la herufi tatu nitakaloliuliza kusanyiko, usiku wa leo.

*Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu?
mbona, basi, haijarejea afya ya binti ya watu wangu?*

¹⁰² Sasa, nitaauliza hilo swali kama Mungu alivyouliza: *Mbona?* M-b-o-n-a. “Mbona haijarejea afya ya binti ya watu Wangu?” [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.) Sasa, hilo ni tamshi kwelikweli, lakini ninaamini ya kwamba kama Mungu akifanya njia kwa ajili ya chochote, akifanya njia ya kuepukia, akifanya njia kwa ajili yake, wala watu hawalipokei, hawatembeji humo, basi Yeye ana haki ya kuuliza, “Kwa nini?”

¹⁰³ Kama ulienda na kumnunulia mvulana wako gari, useme, “Sasa, Kadogoo, si—sitaki u—uende kwenye vyumba vyovyote vya kamari, baba na mama yako, sisi ni nyumba ya Kikristo, Sitaki uvute sigara, Sitaki uende kwenye madansi pamoja na hizi ngoma za kisasa ambamo wanakunywa pombe na kadhalika. Si—sisi ni Wakristo hapa, Kadogoo, nawe uta—utaleta aibu juu ya nyumba yetu, na juu ya huduma tunayosimamia. Nami nitakuwa mwema sana kwako, Kadogoo. Mimi... Baba anafanya kazi kwa bidii, kwa hiyo nitatoa jasho mpaka nitakapoweka pesa za kutosha kukununulia gari dogo, maana unaweza kwenda shuleni nayo, wewe na Dadako, na—na mwe wazuri tu. Nitakununulia nguo nzuri.”

¹⁰⁴ Halafu unakuta kwamba Kadogoo anavuta sigara, na kunywa pombe, na kutangatanga, basi una haki ya kumwuliza mvulana huyo, “Kwa nini?” kwa sababu ulimtengenezea kila njia ya kujifurahisha, na kuchukua maskini gari lake, kwenda kuvua samaki, na—na kadhalika, na kwenda kuliendesha. Ndi—ndipo

basi ungekuwa na haki kama baba kumwuliza, “Kwa nini? Kwa nini ukafanya hivyo?” Hiyo si ni kweli, ndugu?

¹⁰⁵ Basi kama Mungu akifanya njia kwa ajili ya watu Wake kuepukia, na kuiondokea ile hasira iliyo karibu, nao hawalipokei, basi Yeye ana haki ya kuuliza ni kwa nini hawakulipokea.

¹⁰⁶ Nilitua Bombay, India, hapa wakati fulani uliopita, nami nilikuwa nikisoma makala kwenye gazeti, ningali ninayo, ama, samahani, Tommy Nickel anayo sasa, yanatoka katika *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo, na kusema, “Hapana shaka tetemeko la nchi limekwisha.” Sasa, India si matajiri, kama walivyo Marekani. Sasa, wageni kweli wanafikiri ya kwamba maadamu wewe ni Mmarekani, wewe ni tajiri, vema, hilo ni kweli kwa mujibu wao, lakini, kulingana na hali ya mazingira inayowabidi kuishia. Lakini wa—wana nyua zao ambapo wanaokota mawe, kama tulivyofanya katika Marekani ya mwanzoni, kutengeneza nyua zao. Zao, nyumba zao nyingi zimejengwa kwa mawe na matope.

¹⁰⁷ Lakini siku moja jambo la kigeni lilitokea, ndipo maskini ndege wote walioishi kwenye miamba hii kando ya nyua, na katika minara mikubwa, wote waliruka kutoka kwenye kiota chao, na kukiacha, wakakihamisha tu kiota chao. Nao ng’ombe na kondoo ambao, joto lilipoingia, wangekula asubuni na mapema, na jioni sana, lakini badala yake, halafu katika joto la mchana, wangekuja na kusimama kwenye vivuli vya ua huu wapate baridi, lakini badala yake, walikimbilia moja kwa moja katikati ya uwanja, ndipo wote wakaegemeana wao kwa wao, ng’ombe, kondoo, wanyama.

¹⁰⁸ Nao watu wakashangaa, “Ni tendo la kigeni jinsi gani hili!” Siku mbili lilitukia. Mara tetemeko la ardhi likaipiga hiyo nchi, hizo kuta zikaanguka. Hilo tetemeko la ardhi likatikisa mara nne ama tano mbalimbali kwa, labda, siku mbili walikuwa na tetemeko la ardhi moja baada ya lingine. Hatimaye, maskini ndege hao wakaanza kuruka kurudi kwenye kiota chao, mahali paliposalia, ng’ombe wakarudi karibu na kuta zilizosalia. Ilikuwa ni kitu gani? Mungu yeye yule aliyewaonya wale ndege, na wanyama kuingia ndani ya safina kwa ajili ya usalama, inaonyesha Yeye ni Mungu yeye yule leo. Mnaona? Aliwaonya wanyama Wake wakimbie, na waondoke kwenye hizo kuta kubwa zilizokuwa karibu kuanguka.

¹⁰⁹ Sasa, kama Mungu anaweza kufanya hivyo, kwa silika, kwa mnyama, ni zaidi sana vipi sisi, tunaodai kuwa watoto Wake, tuliojazwa na Roho Mtakatifu, kuonywa na Roho kuyakimbia mambo haya ya ulimwengu, kuyaacha? Yanakaribia kuporomoka, tuingie kwenye Safina ya usalama, ambayo ni Kristo, upesi uwezavyo kuingia ndani Yake, nenda upesi. Usingoje hata dakika moja, kwa maana saa inakuja ambapo

mlango utafungwa, na rehema haitakuwako tena. Kwa hiyo, kama Mungu amefanya njia, na halafu kwenye ile Hukumu Yeye atauliza, “Kwa nini?”

Nilikuwa nikijua wimbo tulioimba:

Kitabu cha mwisho kitakapofunguliwa—Vipi basi?

Wakati mhubiri amehubiri maombi yake ya mwisho, ama, ameomba maombi yake ya mwisho (Kitu kama hicho.), Biblia imefungwa mimbarani,

Silaha zote zimelundikwa, ving'ora vya kuzima taa vimelia mara yake ya mwisho juu ya kilima,

Kurudi nyuma kumekamilika, jua linatua kwa mara yake ya mwisho,

Mwi—mwigaji amefanya kitendo chake cha mwisho, na Hollywood imekwisha—Vipi basi?

Utaombwa utoe sababu kwa nini hukuja—Vipi basi?

Utajibuje? Utaepukaje?

¹¹⁰ Sasa, tunataka kuwazia mambo haya kwa uzito kwa yapata dakika thelathini, ninapojaribu kurejea kwenye Maandiko fulani hapa. Sasa, mtaulizwa, kila mmoja wenu, “Kwa nini?” Inapofikia mahali ambapo Mungu amefanya kila maandalizi, akamtuma Roho Mtakatifu, na kufunua, na kuonyesha kila kitu alichohidi katika Biblia papo hapo mbele zako, basi utafanya nini?

¹¹¹ Mwajua, ni kitu kama hivi majuzi huko Louisville, Kentucky, kulikuwa na mwanamke aliyekuwa na mtoto mchanga, naye alikuwa akimbeba mahali mahali, naye alikuwa katika duka la bei rahisi, naye angesema, “Angalia, Kipenzi! Angalia, Kipenzi! Angalia, Kipenzi!” Ndi—ndipo akashikwa na mpagao, halafu baada ya kitambo kidogo akasema, “Loo!” Akapiga mayowe tu.

¹¹² Nao watu, walinzi hu—humo jengoni wakaanza kuona lile tendo geni la mwanamke huyo. Naye akaangukia tu mezani, na kusema . . . akaanza kulia. Basi waliposhangaa alikuwa na shida gani, wakaenda pale.

¹¹³ Akasema, “Mvulana wangu mdogo hapa, mwenye umri wa miaka miwili,” kasema, “yapata miezi sita iliyopita, aliketi tu na kukodoa macho.” Kisha kasema, “Nilimpeleka kwa daktari. Hakuna kitu kinachopaswa kumvutia mvulana mdogo kama yeye, kitakachomvutia.” Kasema, “Yeye huketi tu na kuzubaa.” Kisha kasema, “Ninatikisa vitu hivi vidogo na kadhalika ambavyo vinapaswa kuvutia usikivu wake, bali anakaa tu amezubaa. Ana kasoro.”

¹¹⁴ Sasa, samahani kama mimi... Sikusudii kuumiza hisia, lakini kumbukeni, hapa ndipo yalipo masahihisho, hii ni hukumu. Hiyo zaidi sana ni kama kanisa lilivyo siku hizi. Mungu ametikisa kila namna ya karama za kiroho mbele zao, nao bado wameketi kana kwamba walikuwa tu wamezubaa, hawajui. Unaweza kuwakemea wanawake waliokata nywele zao, kamwe hawafanyi lolote kulihusu; kuhusu kuvaa... kuvalia kizinifu, kamwe hawafanyi lolote kulihusu; kuhusu kuzozana katika madhehebu, moja ni bora kuliko *hili*, na *hili* ni *hivi*, na *hili* ni *hivi*, hawafanyi lolote kulihusu, wanaendelea tu kuzozana vivyo hivyo. Sijui tutafanya nini kwenye ile Hukumu wakati Mungu atakaposema, “Kwa nini?”

¹¹⁵ Alimtuma Oral Roberts, Tommy Hicks, kanena kwa lugha, na kufasiri lugha, na kutoa jumbe, na manabii, na chochote kile alichohidi katika Biblia, na kila baraka, Yeye aliitikisa mbele ya kanisa, na daima, wanagaagaa katika kutokuamini. Ndipo Mungu atasema, “Kwa nini?” Basi jibu lako ni nini?

¹¹⁶ Sasa, msi—msifikiri ninajaribu kuwadhuru, lakini angalieni wameketi pale kwenye viti vya magurudumu, angalieni huko kwenye magonjwa. Mara nyingi kama Oral Roberts, na wahudumu wengi mashuhuri wa karama za uponyaji, na kina Jack Coe, na kadhalika pamoja na hiyo imani ya mbwa mkubwa mkaidi, wakiishikilia, nanyi mmeona mambo yakifanywa, ndipo akaja na karama ya kinabii, na huonyesha, na hupambanua, na kuweka mathibitisho yasiyokosea ulimwenguni kote, ndipo wanaketi, na kusema, “Vema sasa, sijui kama jambo fulani lingeweza kutukia?” Mungu atawauliza, “Kwa nini?” Nanyi itawabidi kujibu. Sasa, hiyo ni kweli.

¹¹⁷ Sasa, wakati mmoja kulikuwako na mfalme, jina lake lilikuwa Ahazia, alikuwa mwana wa Yezebeli na—na Ahabu. Naye akachukua mahali pa baba yake huko Samaria wakati Ahabu alipouawa kulingana na manabii, nao mbwa wakairamba damu yake, yale hasa nabii aliyokuwa amesema yangetukia. Basi Ahazia akapachukua mahali pake, naye alikuwa ni mwasi, kama tu baba yake, na mamake.

¹¹⁸ Basi siku moja alikuwa akitembea kwenye dirisha la nyumba yake, labda, dirisha lile lile ambalo yu—yule malkia wa Sheba, au mwingine... katika siku zake ambapo wao, walipolijenga hekalu la Sulemani, naye a—akaangukia kupitia dirisha hilo, na kujeruhiwa, ndipo akaugua. Ndipo akatuma watu hadi Ekroni, kwa Baal-zebubu, ibilisi, akawatuma watu wawili kule juu, ama, kundi la watu, kasema, “Kweeni mkafanye shauri, mkamwulize Baal-zebubu, mungu wa—wa Ekroni, kama nitapona, ndivyo au sivyo.”

¹¹⁹ Ndipo Mungu akamtuma Malaika huko chini kwa maskini Eliya aliyeketi huko chini kwenye mlango mdogo wa pango, Akasema, “Kwea ukaonane nao.” Mungu anajua wakati wa

kutuma na wakati wa kutotuma. Kasema, “Kwea ukawakabili, ukawaambie, BWANA ASEMA HIVI.”

¹²⁰ Ndipo maskini Eliya akatembea kwa ukali kule, akasimama barabarani. Alipowaona wakija, akasema, “Mko njiani kuelekea huko. . . kuelekea—kuelekea Ekroni huko, tukikimbia huku na Baal-zebubu, kukutana na manabii wao, kutaka kujua kama Ahazia atapona au la.” Kasema, “Rudini mkamwambie, ‘Kwa nini ukafanya hivyo? Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Ni kwa sababu hakuna nabii kule? Kwa nini ukiendee kitu kama hicho basi?’ Nendeni mkamwambie BWANA ASEMA HIVI, hatatoka kwenye kitanda hicho.” Loo, jamani! Huyu ni Mungu.

¹²¹ Kuna shida gani kwamba tunabadilisha makaratasi yetu kutoka Methodisti, hadi Baptisti, hadi Presbiteri, na madhehebu mengine yote mbalimbali na kadhalika, tukikimbia huku na huku? Kwa nini tunafanya mambo haya? Kwa nini tunaenda. . . ? Kwa nini tunakaa nyumbani Jumatano usiku kutazama *Tunampenda Susi*, ama baadhi ya hiyo michezo, na vipindi vya televisheni, na mambo kama hayo? Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Pentekoste? Je, ni kwa sababu hakuna furaha katika nyumba ya Bwana? Ni kwa sababu hakuna nabii huko? Ni kwamba mambo haya sivyo yalivyo?

¹²² “Huko hakuna tabibu? Hapana zeri katika Gileadi?” Zeri ni uponyaji. “Basi mbona binti ya watu Wangu angali ni mgonjwa?” Anauliza ni kwa nini. Kwa nini tunafanya mambo haya? Mbona tunatenda kama ulimwengu? Mbona wanawake wetu wangali wanavalia kama walimwengu? Mbona wachungaji wetu wanawaacha mashemasi waingie na wake wawili au watatu mbalimbali, na kutumika katika halmashauri ya mashemasi? Mbona tuna. . . tunaenda tu kama ulimwengu, na kuanza kutenda kama ulimwengu, na kuzungumza kama ulimwengu, na—na, kwa nini tunafanya hivyo? Ni kwa sababu. . . ?

¹²³ Kwa nini inatubidi kujenga madhabahu makubwa ambayo yana thamani ya mamilioni na mamilioni ya dola, na kuhubiri Yesu anakuja siku chache zijazo? Wamishenari hudumani bila viatu miguuni mwao, wakiishi kwa mlo mmoja kwa siku! Kwa nini tutupe pesa zetu kwa vitu kama hivyo, huku wamishenari ninaowajua hawana viatu miguuni mwao? Enyi watu wa Mungu, tutawajibika kwa hilo siku moja. Mungu atasema, “Kwa nini?” Hiyo ni kweli. Mama, yeye akijaribu kukupa mtoto mchanga, huku maskini tumbo lake limevimba *hivyo*, akifa kwa njaa. Tunajaribu na tunataka kushindana na kina Jones. Mungu atatuuliza, “Kwa nini?”

¹²⁴ Sasa, shirika letu kuu linajenga majengo yenye thamani ya makumi ya mamilioni ya dola, na vitu kama hivyo, ati na kuhubiri Yesu yuaja hivi karibuni? Ushuhuda wetu wenyewe unatukabili usoni, kwa Neno, la hatuamini tunachozungumzia.

Imekuwa tu ni kawaida, kuzunguka, na kuzunguka, na kuzunguka. “Baba anasema, kwa hiyo nasi tunasema hivyo pia.” Kama kweli unaamini, tenda hivyo.

¹²⁵ Kama unaamini katika uponyaji wa Kiungu, mkubali Yeye. Kama unaamini Roho Mtakatifu ni sahihi, kaa hapo, si kwa dakika kumi, mpaka atakapokuja, usichukue kibatala chochote. Kaeni hapo mpaka Kitu halisi kitakapokuwapo. Vema, mmepita kutoka mautini kuingia Uzimani, ndipo ndugu ndege wataimba tofauti, kila mtu, wote uliowachukia, utawapenda, na kila kitu kitakuwa tofauti utakapofanya hivyo.

¹²⁶ Kwa nini tunaweka kitu badala yake? Mungu atasema, “Kwa nini?” Ndipo itatubidi kujibu. Sasa, hiyo ni kweli, ndugu, mnaamini hilo, nyote mnaamini, ninyi wanaume. Sasa, hapo—hapo ndipo tunaposimama. Tunapaswa kuwa Kanisa linalowaka moto kwa imani, ndugu, tukiwaka moto, jamani, jamani, badala yake sisi kidogo ni kama kundi la mbwa mwitu waliosukumwa pembeni, “Vema, uh, naam, ninaamini hilo, uh-huh.” Unarudi nyuma, simama hapo, ana kwa ana kwake.

¹²⁷ Kama sisi ni Wapentekoste, tuwe Wapentekoste. Kama sivyo, kwa nini tusivunje tu kitu hicho, tuungane na baadhi ya madhehebu yetu mengine, ndugu zetu Wamethodisti hapa, ndugu zetu Wabaptisti, Wapente-... , ama, Presbiteri yetu, au, kwa nini ninyi nyote msirudi muwe Wakatoliki? Hilo ndilo lenye umri mkubwa kuliko yote ya kundi lao, mnaona, rudini na muwe hivyo. Lakini kama sisi ni Wapentekoste, hebu na tuwe Wapentekoste kwa tukio. Inukeni, jitikiseni. Naam. Kasema, “Nendeni mkamwambie, ‘Kuna nini?’” Kwa nini Wapentekoste...?

¹²⁸ Msichana mmoja aliniuliza hivi majuzi, kasema, “Ndugu Branham, wameanza kuvaa sketi za kashfa.”

Nikasema, “Ni kitu gani hicho?”

¹²⁹ “Loo,” akasema, “wasichana wanavaa sketi zilizokatwa hivi zinazoonyesha nguo zao za ndani. Unafikiri ni kosa kwa msichana kufanya hivyo?”

¹³⁰ Nikasema, “Dada, msichana Mpentekoste, aliyejazwa na Roho Mtakatifu anataka kuonyesha sketi yake ya ndani kwa nini? Ningetaka tu kukuuliza hilo.” Mnaona? Kama angalikuwa sawa na Mungu, haingemlazimu kuuliza hilo.

¹³¹ Nina Biblia ndogo, nilipoanza kwa mara ya kwanza niliandika kitabu kidogo, kunaweza kuwa na mtu atakayesema, “Je, ni vibaya kuvuta sigara, ni vibaya kunywa pombe, ni vibaya kufanya *hiki-na-hiki*?” namna hiyo. Nikasema, “Usiniulize maswali ya kipumbavu, liweke hili mawazoni mwako, kama unampenda Bwana kwa moyo wako wote, huvuti sigara, hutafuni tumbaku, wala kunywa pombe yoyote haramu.” Na hilo, ningali ninashikilia hilo. Wakati upendo wa Mungu ukiwa

moyoni mwako, huna wakati kwa ajili ya kitu kingine chochote, umejisalimisha.

¹³² Biblia inasema, “Ukiipenda dunia, ama mambo ya dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Na maisha yako yenyewe yanaonyesha hivyo. Natumaini hilo ni dhahiri vya kutosha, haitanibidi kuwa dhahiri zaidi. Mnaona? Lakini hiyo ni kweli, “Kwa matunda yao mnaajua hilo.”

¹³³ Kwa hiyo tujitikise, hebu na tuwe Wapentekoste, ama—ama tuwe kitu kingine. Sisi si Wapentekoste, hebu tuache kusema ndivyo tulivyo, mnaona, mpaka tutakaporudi kwenye tukio halisi la Kipentekoste, turudi kwenye imani, imani jasiri. Hao wanafunzi walitia muhuri kifo chao kwa imani yao. “Loo, imani ya baba zetu, ingali hai, licha ya gereza, mwali wa moto, au upanga.” Hiyo ndiyo tunayotaka, imani halisi, ya kweli.

¹³⁴ Ninyi Wamethodisti mnaihitaji, ninyi Wabaptisti mnaihitaji, ninyi Wapentekoste mnaihitaji, sisi sote tunaihitaji. Mungu atasema, “Kwanini? Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Basi kwa nini? Je, hakuna—hakuna nabii katika Israeli? Huko hakuna Mungu? Hivi Wapentekoste wamempoteza Mungu wao? Hivi hawana karama zingine zaidi miongoni mwa Wapentekoste? Hawana manabii tena, karama za unabii, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti, hakuna mwingine wa kunena kwa lugha na kutoa ujumbe?” Jambo moja, hamziheshimu karama hizo vya kutosha, jambo lingine, hamzithibitishi kwanza, ndipo mnapata kila namna ya roho mle ndani ikinena. Mnapopata roho hiyo ambayo haisemi jambo lililo sahihi, iondoeni humo, hamtaki kibadala, Mungu ana kilicho halisi kwa ajili yenu.

¹³⁵ Mtu fulani akinena kwa lugha, basi mwacheni, ni ujumbe kwa kanisa, kila mtu atulie, huyo ni Mungu akinena. Basi msikilize mwone, kama si kwa ajili ya kanisa, basi ni la kimwili. Mnaona? Kama ni jambo fulani kwa kanisa, wala halitimii, basi huyo ni roho mwovu, mchafu, maana Mungu hasemi uongo. Nanyi mtaweka kanisa lenu katika utaratibu. Mnaona?

¹³⁶ Lakini jinsi ilivyo, mnaliachilia tu liruke popote, huku mtu fulani akitafuna chingamu, na mwingine akila bisi, mmoja akizungumza, mwingine akinong’oneza, mtu mmoja akijaribu kunena kwa lugha, watatu ama wanne kwa wakati mmoja, na—na *huyu* akijaribu. . . Loo, jamani! Linakuwa jambo la Wakorintho tena. Tunapaswa kuirejesha katika utaratibu, kuirudisha kwa Roho Mtakatifu, kuijaribu karama hiyo.

Mnasema, “Loo, Ndugu Branham, tunajaribu hilo, pia?”

¹³⁷ Vema, ndugu, haina budi kujaribiwa papa hapa, sivyo? Hiyo ni—hiyo ni kweli. Msiogope, kama ni Mungu, ni kweli, asilimia mia moja. Lakini. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . moja kwa moja juu ya hiyo.

¹³⁸ Nilikuwa nikizungumza na mtu huyo, mhariri, Bob *jina-lake-nani*, anayeandika *Maisha ya Kikristo*, naye alikuwa huko chini kwenye...Shu-..., la, si Bob Shuler, ni yule ndugu Mmethodisti. Ninamjua vizuri sana, bali siwezi kukumbuka jina lake, ambaye huandika *Maisha ya Kikristo*, nanii...Walker. Alikuwa Indianapolis, naye akasema, “Ndugu Branham, vipi kuhusu Wapentekoste?” Akasema, “Wanafanya *hivi* na kufanya *vile*?”

¹³⁹ Nikasema, “Na hao wengine je? Wanafanya jambo lile lile. Lakini mara nyingi washiriki wao wako kwenye gazeti, wako huko nje, wahiriri wa gazeti, na kadhalika, husikii habari zake,” bali nikasema, “wanafanya vibaya vivyo hivyo.” Lakini nikasema, “Wakati mwingine mtu hushika njia mbaya, ndipo basi ninyi nyote mnafanya nini? Mnaruka moja kwa moja ng’ambo ya kile kitu halisi, na mnaliendea hilo. Huku hiki upande *huu*, hicho ndicho moto wa kigeni kweli, utalimimina moja kwa moja kurudi kwa ya kale, baridi.” Nikasema, “Ni moja kwa moja katikati ya barara, anapitia Roho Mtakatifu halisi, Kanisa.” Utukufu! Hao wa kale, baridi wa kawaida, upande mmoja, na wa kigeugeu upande huo mwingine, wametokana na cha halisi.

¹⁴⁰ Isaya alisema, katika mlango wa 35, “Kutakuwako na njia kuu,” nanyi Wanazarayo mnaia “njia kuu ya utakatifu,” mmekosea. Sio kulipinga neno lenu, bali alisema, “Kutakuwako na njia kuu, na,” *na* ni kiunganishi, “kutakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa,” si njia kuu, bali, “*njia* ya utakatifu.” Katikati ya barabara.

¹⁴¹ Dk. Wead, ninajua ninyi ndugu wa Assembly mnamjua, ye—yeye ni ndugu mpendwa sana, rafiki yangu mpendwa. Nilikuwa nikihubiri juu ya hilo wakati mmoja, Ndugu Wead akasimama, akasema, “Mnajua nini?”

¹⁴² Ndugu Vibbert, nadhani ninyi nyote mnamjua Ndugu Vibbert, yeye ni binamu yangu, yeye ni Mwassemblies mkubwa huko—huko Evansville, Indiana, sisi tukiwa na mkutano wa wanaume kule.

Kasema, akasema—akasema, “Ndugu Branham alizungumza kuhusu ‘katikati ya barabara,’” kasema, “hayo si maadili mazuri ya kuendesha gari.”

¹⁴³ Kwa hiyo, ilitokea kwamba nilikuwa nimesimama nyuma yake, yeye hakujua, Nikasema, “Unaona, Ndugu Wead, jinsi tu mnavyoweza kuwa wa kidunia, ninyi ndugu wa Assembly?” Yeye ni ndugu wa thamani, na Assemblies ni mojawapo ya wadhamini wangu wakuu. Kwa hiyo, nikasema, “Unaona, mnawazia tu juu ya mambo ya duniani sana, ndipo mnachanganyikiwa kabisa, hata yote mnayoweza kuwazia ni mambo ya duniani tu.” Nikasema, “Hakika, papa hapa duniani hayo ni maadili mabaya,

lakini barabara hii ninayozungumzia, hurudi nyuma, ni tiketi tu isiyo na kurudi.” Na kwa hiyo tukacheka tu.

Ni wangapi wanaomjua Roy Wead? Ye—yeye ni mmoja wa watu wazuri sana ungeweza kuwapata; amekuwa ndugu halisi kwangu. Na basi iko hivyo.

Lakini Mungu atatuuliza, “Kwa nini?” Alimwuliza huyo mfalme, “Kwa nini?”

¹⁴⁴ Sasa, si kwamba hawakuwa na nabii ambaye angeweza kumtaka shauri. La, la. La, bwana. Angeweza kwenda na kumtaka shauri nabii wa Mungu. Haikuwa kwa sababu hakukuwa na Mungu katika Israeli, hakika, Mungu wa Israeli angemwambia nabii kuhusu huyo mfalme. Lakini ilikuwa ukaidi wa mfalme mwenyewe.

¹⁴⁵ Na hiyo ndiyo shida ya mataifa, siku hizi, ulimwenguni. Si kwamba hatuna Mungu, bali sayansi inajaribu kumwondosha jukwaani, nao watu ni wakaidi sana hawawezi kusimama juu ya kanuni za Neno la Mungu. Kweli kabisa.

¹⁴⁶ Wanasema, “Loo, hilo ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha.” Na liwe liwalo. Nimekuwa... Nimesafiri kote ulimwenguni, mara kadhaa, sijawahi kumwona mtakatifu anayejibingirisha bado, nimetafuta. Kuna mashirika mia tisa na sitini na tisa mbalimbali pamoja na makanisa yaliyoorodheshwa huko Washington, wala hakuna hata moja la hayo linaloitwa *Watakatifu Wanaojibingirisha*. Hilo ni jina chafu ambalo ibilisi aliliwekelea Kanisa. Hakuna kitu kama *mtakatifu anayejibingirisha*, hakuna shirika kama hilo linaloitwa *Watakatifu Wanaojibingirisha*. Wanamwita mtu yeyote anayeamini katika utakatifu *mtakatifu anayejibingirisha*. Na kama... “Pasipo utakatifu, hakuna mtu atakayemwona Mungu.” Kwa hiyo mnaona asili yake ni wapi. Naam.

¹⁴⁷ Vema, mfalme, alikuwa mkaidi tu, hakutaka kumsikiliza nabii. Walikuwa na nabii, walikuwa na Mungu, lakini m—mfalme alikuwa mkaidi sana. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, watu ni wabinafsi kupita kiasi. Wanazungumza juu ya uponyaji wa Kiungu, afadhali wakae huko nje na wafe, kuliko hata kukubali waliamini katika uponyaji wa Kiungu. Watu wangependelea...

¹⁴⁸ Ni kama tu mtu anayekufa kwenye vipandio vya mlango wa daktari kwa sababu hatakuwa dawa yake. Daktari ana dawa ya ugonjwa alio nao, naye huyo mtu ataketi kwenye ngazi ya mlangoni, huku daktari akiwa na dawa nyingi, wala hatainywa, mkaidi sana hawezi kuingia na kuinywa. Atakufa, anapaswa kufa, hivyo basi, kama akijisikia hivyo kulihusu.

¹⁴⁹ Si kwa sababu daktari... Usimlaumu daktari. Kama daktari ana dawa na yuko tayari kuitoa, huku mgonjwa ameketi mlangoni, na ni mkaidi sana asingeweza kuingia kuinywa, usimlaumu daktari, si kosa la daktari, wala si la dawa, ni kosa la huyo mgonjwa, hatainywa.

¹⁵⁰ Ni jambo lile lile kanisani. Tuna zeri nyingi sana huko Gileadi, na tuna madaktari hapa, bali watu wanakufia kwenye marefu ya kanisa bila Roho Mtakatifu, kwa sababu wao ni wakaidi sana kuja kuinywa, nao wanahofu itaathiri heshima yao ya kijamii, itawavunja, huenda ikawagharimu sehemu ndogo ya karamu zao za kadi na kadhalika, wakihofia huenda wakakata kidogo, na kufanya utundu. La, usimlaumu daktari, usiilaumu tiba, laumu tu huyo mgonjwa kwa kutoichukua hiyo tiba. Hapo ndipo lilipo.

¹⁵¹ Tuna dawa, tuna nyingi. Ulimwengu umejaa Roho Mtakatifu, Yuko tu kila mahali. Tunao matabibu, ndugu, wanaojua jinsi ya kutoa dawa, bali wa—watu hawatainywa. “Loo,” wanasema, “Mimi ni Mpresbiteri.” Hilo halimaanishi zaidi ya vile nguruwe angeweza kuvaa tandiko la kike kwenye zizi la farasi wa mashindano. Hilo halina uhusiano wowote nalo, halina uhusiano wowote nalo. Presbiteri, Methodisti, Baptisti, au dhehebu la Kipentekoste, ama chochote kile hakimaanishi *hivyo* kwa Mungu. [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.] Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Wanakufia kwenye marefu ya kanisa, si kwa sababu hakuna dawa, dawa ni nyingi, bali ni kwa sababu wanakataa kuinywa.

¹⁵² Sasa, mnajua nini? Ukikataa kunywa dawa ya daktari, ni hatari, huenda ukafa usipoinywa dawa ya daktari, huenda ukafa, na hiyo ni hatari kutoinywa, kama vile ile chanjo ya Salk, kama ndui.

¹⁵³ Ninapoenda nchi za ng’ambo na—naamini wa—wao hunindunga sindano nyingi sana mpaka ninaonekana kama yai la kanga, kusafiri sehemu nyingi, ambapo wao, wananinii tu, wananidunga ya homa ya manjano, na—na kila namna ya dawa wanasema ambayo inakuepusha kuinywa. Sikutaka kudungwa, bali inakubidi kudungwa kwa vyovyote vile, kwa hiyo hilo ni sawa.

¹⁵⁴ Unasema, “Ndugu Branham, unaamini katika dawa?” Mbona, hakika, bila shaka. Ni vitu vilivyotolewa na Mungu, tunaamini hilo, bali hayo siyo yanayokuponya. Vipi kama hatukuwa na afya na usafi, tungekuwa na nini? jinsi watu walivyoongezeka duniani siku hizi, na ni vitu vingapi. Kama hospitali si ya Mungu, basi kiteketeze kitu hicho, ni upinga-Kristo. Mnaona? Hakika, bali ni ya Mungu, bali haziponyi, ni mahali tu pa kukuweka kando, na kukusaidia, na kujaribu kuwadumisha safi wakati. . . Kama umewahi kuponywa, Mungu alikuponya.

¹⁵⁵ Daktari maarufu, nisingetaja jina lake, yeye aliniambia, akasema, “Billy, ingia humu, na jambo la kwanza,” kasema, “daktari wa farasi hana budi kuwa na akili zaidi kuliko sisi.” Kasema, “Hana budi kujua mahali farasi ni mgonjwa.” Kasema, “Unaingia ndani, kasema, ‘Una shida gani?’” Kasema,

“Wewe niambie kuna shida gani.” Kasema, “Nina haraka, nitakuandikia maagizo kidogo.” Kasema, “Unaona ni jina la nani lililoko hapo? Mwuza dawa, aliilipia hii.” Kasema, “Nitakutoza dola kumi. Nenda kule ikajazwe, naye atarudi na kuijaza, naye anakutoza dola tatu kwa kitu alicholipia senti mbili.” Kasema, “Utainywa kwa siku tatu ama nne,” kasema, “iwapo Bwana hajakuponya kufikia wakati huo, wewe rudi ofisini mwangu, nitakutoza dola tano zaidi, na kusema, ‘Nenda ukairudie tena.’” Mnaona, haya basi. Mungu ndiye aponyaye.

¹⁵⁶ Sasa, simhukumu daktari mzuri, Mungu anajua hilo. Nami ninasema jambo hili moja, hebu nisimame kwa dakika moja, Nimeona madaktari wengi zaidi wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu kuliko wahubiri nilio nao, hiyo ni kweli, nami nimeenda kutoka hospitali moja hadi nyingine.

¹⁵⁷ Daktari maarufu aliniagiza niende kwa mzee mmoja hivi majuzi, huyo ni daktari mzee, bali sina wakati wa kuwaambia, aliyekuwa na umri wa miaka themanini, alikuwa amepoteza fahamu kwa majuma mawili. Ndugu Goad hapa anajua kisa hicho, ilitokea kwamba ni wa klabu ile ile, klabu ya kurusha risasi ambayo ndiyo kwanza niingie siku chache zilizopita. Huyo daktari mzee alikuwa amelala pale, na ni mtu maarufu, mmoja wa madaktari walio bora sana huko kusini. Kasema, “Ndugu Branham, utakapokuja huku, zungumza tu na huyo mzee.” Alikuwa amepoteza fahamu.

Na wakati nilipokuwa nimeushika mkono wake, alipata fahamu, na kusema, “Halo, Daktari.”

Nikasema, “Mimi si daktari,” nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

Akasema, “Vema, aisee, hapana shaka nilikuwa nimelala.” Naam, yapata majuma matatu.

Nikasema, “Nadhani, Daktari. Umekuwa ukifanya matibabu kwa muda gani?”

Kasema, “Una umri gani?”

Nikasema, “Umri wa miaka hamsini na miwili.”

Akasema, “Kabla hujaanza kunyonya.”

¹⁵⁸ Nami nikasema, “Nadhani usiku mwingi umekuwa na tochi kwenye kingo za kijito,” maskini daktari wa mashambani, “ukishuka kwenye kingo za kijito, ukijaribu kutafuta mtoto mchanga anayeumwa na tumbo, au mama katika utungu wa kuzaa.”

Naye akasema, “Sio tochi, taa.”

Nami nikasema, “Nakisia wewe, wakati huo hukupata kitu kwake, labda mayai kadhaa, ama kitu fulani.”

Kasema, “La, sikutarajia chochote.”

Ndipo nikasema, “Vema, unajua ninachowazia, Doc? Unamwamini Mungu?”

Akasema, “Nisingekuwa hapa kama sikumwamini.”

¹⁵⁹ Nami nikasema, “Unajua ninachofikiria?” Nikasema, “Huko katika nchi ya Utukufu, hapana shaka wana mahali padogo pembeni, ambapo maskini hao madaktari wazuri wote wa kale ambao wamesaidia mara nyingi sana. . .” Akaanza kulia, nikasema, “Sasa, ninakuchangamsha.”

Akasema, “La, la, la, kaa papa hapa.”

¹⁶⁰ Daktari, daktari wangu akisimama pale, rafiki yangu, amesimama, akiminya mikono yake, akilia, amesimama nyuma pembeni. Baadaye akasema, “Sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu.” Kasema, “Ulimfanyia nini?”

Nikasema, “Kamwe sikumfanyia jambo moja, ila kuweka mkono wangu juu yake.”

Mzee mcha Mungu, akasema, “La.”

Nikaushika mkono wake, nikasema, “Nakisia ulifanya upasuaji mwingi, Daktari?”

Akasema, “Kamwe sikukitwaa kisu pasipo kumwomba Muumba wangu anisaidie, na akiongoze.”

¹⁶¹ Nikasema, “Huenda ukawa na umri wa miaka themanini na sita, lakini kama ilinibidi kufanyiwa upasuaji, ningetaka mikono iyo hiyo iufanye.” Hiyo ni kweli. Nikasema, “Lazima kuna mahali padogo huko Mbinguni, ambapo Yeye alikuwa. . .”

Akasema, “Ndugu Branham, unafikiri Yeye ataniruhusu niingie?”

Nikasema, “Nafikiri hivyo.” Akaanza kulia, nikamkumbatia.

¹⁶² Huyu hapa chini kwenye uwanja wa shabaha hivi majuzi, akiwa na maskini gobori kubwa, amesimama pale, akisema, “Angalieni nikipiga shabaha hiyo, enyi wavulana!” Amerudia udaktari, umri wa miaka themanini na sita. Hiyo ni kweli.

¹⁶³ Loo, naam, wana watu halisi mle ndani, na wana wasaliti, pia. Wala msiwakemee, maana tunao wengine, wasaliti, wanaojiita *kasisi*. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa hiyo, sheria ni msumeno, yakata mbele na nyuma. Naam, bwana.

¹⁶⁴ Na watu wana dawa, na—na ile chanjo ya Salk kwa ajili ya watoto hawa wadogo, wala si polio, Ninaomba kila siku ya kwamba Mungu atatutumia kitu fulani kwa ajili ya kansa. Kama hatuwezi kuwa na imani, hebu na tupate kitu kingine, imani ndiyo ya kwanza, hebu tuchague kingine kizuri zaidi, kama hatuwezi kukipata hicho.

¹⁶⁵ Angalieni ulimwengu katika hali uliyomo, maskini, wanadamu wanaoteseke. Msaidie kila mtu uwezaye; kila kitu kinachosaidia ni cha Mungu. Hebu tusaide, hima tufanye

kila tuwezalo, na kuwaombea wanadamu. Jambo la kufanya, ndugu, ni kuunganisha mikono yetu, dawa, madaktari, hospitali, wauguzi, kanisa, na wote pamoja, na tuweke imani yetu katika Mungu, na kusonga mbele, kile tunachohitaji. Mungu atatuuliza mbona hatukufanya hivyo baadhi ya siku hizi.

¹⁶⁶ Mnakumbuka, Luka alikuwa daktari, pia. Sasa, Mungu kamwe hakumhukumu kwa kuwa daktari, lakini, mnakumbuka, aliandika zile hadithi mashuhuri za uponyaji. Ilikuwa ya kushangaza kwake kuona yale Mungu angeweza kufanya, naye ndiye aliyeyaandika, “Kitabu cha kwanza, Ee Theofilo, nimekuandikia,” na kadhalika, namna hiyo, “ya Yesu wa Nazareti, yale yote alioanza kufanya na kusema.” Alijua kile Yesu alichokuwa.

¹⁶⁷ Sasa, watu wakifa kwenye marefu ya kanisa kwa sababu wanakataa tiba. Sasa, ni jambo la hatari kukataa hiyo. Lakini ni jambo la hatari zaidi jinsi gani kukataa Zeri ya Mungu? Zeri ya Mungu ni nini? Roho Mtakatifu, hiyo ndiyo Tiba ya dhambi. Huenda ukakataa dawa ya daktari, nawe huenda ukaendelea, na kuishi saa moja ya kawaida, ama juma moja, ama mawili, ama, na kufa, na kuendelea. Huenda ukafanya hivyo, huenda ukafupisha siku zako, bali kama ukiikataa Dawa ya Mungu utakufa Milele, utatengwa kabisa na Mungu na rehema milele. Kwa hiyo kamwe usininii . . .

¹⁶⁸ “Hivi hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Basi binti ya watu Wangu ana shida gani hata hawawezi kuamini katika uponyaji wa Kiungu tena? Ni kwa sababu haufundishwi?”

“La.”

“Vema, kuna shida gani basi? Kuna shida gani na ubatizo wa Roho Mtakatifu, wameacha kuufundisha?”

“La.”

“Kupata . . . Je, watu waliupata?”

“Naam.”

“Vema, kuna zeri nyingi sana?”

¹⁶⁹ Yeyote atakaye, na aje, anywe kwenye chemchemi, chemchemi inayobubujika ya Roho Mtakatifu, akiita, “Yeyote atakaye.” Tabibu akisimama pale kukupitisha kwake. Basi mbona usije? Ndipo Mungu atasema, “Kwa nini? Kwa nini hukufanya hivyo?”

“Unajaribu kufanya nini, Ndugu Branham?” Kuitikisa imani ndani ya watu wapate kutambua.

“Je, hapana zeri katika Gileadi?”

¹⁷⁰ Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Sababu ya wao kuikwepa hoja hiyo, ni kwa sababu wanaogopa kuzaliwa upya, hivyo ndivyo ilivyo. Loo, sisi Wamarekani ni wanamitindo sana, mwajua, loo, jamani, sana. Inatubidi tu kufanya ninii,

kile tunachoita, “majigambo” mwajua. Kila mtu hana budi kuwaiga akina Jones, lakini wana... Natumaini hakuna akina Jones, kama wapo silimaanishi kwao, bali huo ni usemi tu wa Kimarekani kama Doe, John Doe, nitasema. Hawana budi kuwa hivyo, ha—hatuna budi kuwa wa tabaka la juu sana. Wanaogopa kuzaliwa upya. Hebu nikwambie, ndugu! Wanasema, “Loo...”

¹⁷¹ Wakati mmoja nilikuwa huko nje nikihubiri, na kulikuwako na mvulana aliyekuja kutoka kanisa fulani nililokuwa mfuasi wake, akasema, “Billy, unajua nini? Nilikuwa nikifurahia ujumbe wako sana, mpaka yule mwanamke aliposimama huko nyuma na kuanza kupiga mayowe na kulia, kisha akawafanya watu hao wote waanze kulia.”

“Loo,” nikasema, “kwani hilo linakusumbua?”

Akasema, “Mbona, nisingeweza kusikia ulichokuwa ukisema.” Kisha kasema, “Hilo—hilo... Ilikuwa ni sawa kabisa hadi wakati huo.”

Nikasema, “Loo, alikuwa tu akishangilia.”

Kasema, “Loo, hilo lilifanya tu baridi ipite mgongoni mwangu.”

¹⁷² Nikasema, “Ndugu, kama ukiwahi kufika Mbinguni, utaganda hata kufa, hebu nikwambie.” Nikasema, “Kwa sababu hata Malaika Mbinguni wanapiga mayowe huku wameweka mabawa juu ya uso wao, na juu ya miguu yao, mchana na usiku, ‘Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana!’” Nikasema, “Unaishi katika ulimwengu mtulivu sana uliowahi kuishi, ukienda kuzimuni, kutakuwa na kulia na kuomboleza na kusaga meno; ukienda Mbinguni itakuwa, ‘Utukufu! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana,’ mchana na usiku. Katika mahali patulivu sana ulipowahi kuishi.”

Ilitokea kwamba alicheza kwenye timu ya besiboli ya Colgate, naye akasema, “Vema, sininii, hawafanyi hivyo kanisani mwangu.”

Nikasema, “Sasa hilo... Lakini natumaini huwazii lako ndilo kielelezo.”

Na kwa hiyo akasema, “Vema...” Nikasema... Akasema, “Vema, huyo haonekani sana kama Mkristo kwangu, wakati mhudumu anapozungumza kusema jambo...”

¹⁷³ Nikasema, “Unajua nini? Hilo linanitia moyo. Kuwasikia wakisema *amina*, maana yake ‘na iwe hivyo.’” Nikasema, “Nilikuwa na mbwa mmoja.” Nami nikasema, “Angeshambulia chochote ila kicheche.” Nami nikasema, “Ni—ningempeleka kwenye mti chini ya kichaka kilicholundikana, na jambo pekee nililopaswa kufanya lilikuwa ni kumfanya amkamate huyo kicheche, Mimi mwenyewe sikutaka, kwa hiyo...” Nami, hivyo

ndivyo nilivyopata nguo zangu za shule, ilikuwa—ilikuwa ni kwa kutega na kuwinda.

¹⁷⁴ “Na—nami ningemwingiza kicheche huyu chini ya lundo la fito, ndipo maskini Fritz angesimama pale. Jambo pekee nililopaswa kufanya kumfanya aingie chini pale, ainue hilo lundo, naye angerudi nyuma, aniangalie namna *hiyo*, akisema, ‘Bwana, hutanisukumia huko chini, sivyo?’

¹⁷⁵ “Ningesema, ‘Nenda kamkamate, jamani. Mtafute, mtafute, mtafute, jamani. Nenda kamtafute.’ Angeenda kumkamata.” Nikasema, “Ibilisi ndiye kicheche mkubwa sana nimjuaye, ninapowasikia watu wakisema, ‘Hiyo ni kweli, amina,’ tumemsukumia pembeni basi, ndugu, tutampata hivi punde. Mwache tu aende,” hiyo ni kweli. Naam, naam, hiyo ni kweli. Tunaninii. . . Amina.

¹⁷⁶ Nikasema, “Angalia, nilikusikia hivi majuzi usiku wakati Charles Nolan alipoingiza goli hilo, Siishi mbali sana na uwanja huo wa michezo,” nikasema, “si zaidi ya bloku tano.” Nikasema, “Sijawahi kusikia kelele kama hizo maishani mwangu mwote.”

Akasema, “Loo, Billy, laiti ungalikuwa huko!” Kasema, “Kulikuwa na watu watatu kwenye kituo. Nawe unamjua Charles, ulisoma naye.”

Nikasema, “Hakika.”

Kasema, “Aliingiza goli.” Kisha kasema, “Jamani, nakwambia, laiti ungaliwaona wakiingia ndani!”

¹⁷⁷ Nikasema, “Enyi watu msio watakatifu wanaojibingirisha huko chini, hata nisingeweza kulala kwa ajili yenu.” Wasio-watakatifu wanaojibingirisha. Nikasema, “Kama sisi ni watakatifu wanaojibingirisha basi ninyi ni wasio-watakatifu wanaojibingirisha. Unaona?” Nikasema hivyo. Nikasema, “Ungekuwa shabiki duni wa besiboli ukiketi pale, ukisema, ‘Loo, naam, ameingiza goli.’” Nikasema, “Unasema hakusisimkwa sana. Huku ninyi mkiangushiana kofia zenu kutoka kichwani mmoja kwa mwingine, na kupigana kofi, na kutetemeka, na kadhalika namna hiyo.” Nikasema, “Wakati mhubiri anapoingia mimbarani na kuingiza goli namna hiyo, na kuwaona hao watakatifu wakifungua njia, na kuona Mbingu mbele zao, wanapiga makelele, ‘Utukufu! Utukufu! Ninaliona, ninaliona! Haleluya! Haleluya!’” Nikasema, “Wanaanza tu kupanda kwenye barabara kuu ya Mfalme, hivyo tu.” Hilo hapo. Mnaona? Naam.

¹⁷⁸ Loo, naam, wao—wao. . . Ni ajabu jinsi wanavyolikosa, bali nadhani inapaswa tu kuwa hivyo. Yote yameamriwa na Mungu, nami nadhani Yeye. . . hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa.

¹⁷⁹ Sasa, daktari anawezaje kupata dawa ya aina gani hapo ya kumshughulikia mtu, mnaona?

¹⁸⁰ Naam, wanaogopa kuzaliwa upya. Mnajua nini? Sababu ya wao kuogopa kuzaliwa upya, ni kwa kuwa... Sikilizeni, samahani, dada zangu, sivyo? Mimi... mimi... Hili ni kusanyiko lililochanganyikana, bali nyinyi humsikiliza daktari wenu, mimi—mimi ni ndugu yenu. Uzazi wowote ni mchafuko sijali uko wapi, kama uko kwenye zizi la nguruwe, kwenye kitalu, ama ukiwa uko katika chumba kilichopambwa waridi cha hospitali, ni mchafuko, na kuzaliwa upya, pia. Utakufanya ulie kwa maumivu, na kupiga ukelele, kisha uoshe rangi hizo zote kutoka usoni mwako, u—utakufanyia mambo ambayo hukuwazia ungefanya. Utaendelea kama vile hukuwazia ungefanya, ni mchafuko.

¹⁸¹ Lakini unajua, kabla hujazaliwa, huna budi kufa, na watu wengine hufa kwa shida sana, wanarusha mateke, na kupiga kelele, na kupiga mayowe, na kufanya yasiyofaa. “Lakini chembe ya ngano isipoanguka ardhini ikafa, hudumu peke yake.” Kama ukitaka kuzaa tunda, kufa kwa nafsi yako, na theolojia yako ya kujibunia, ukazaliwe mara ya pili kwa Roho na ufufuo. Hiyo ni kweli. Ondoa roho ya kale ya ubinafsi na ukavu ulio ndani yako, chukua Maisha mapya. Ni mchafuko.

¹⁸² Punje ya mahindi isipoanguka ardhini na kuoza, mtu asipooza kwa theolojia yake mwenyewe, isipokuwa umeoza kwa theolojia ya Methodisti, isipokuwa umeoza kwa theolojia ya Baptisti, isipokuwa umeoza kwa theolojia ya Pentekoste, mpaka utakapooza kwa mambo hayo na kujisalimisha mikononi mwa Mungu, basi yule mtu wa kale atakufa, na mtu mpya atazaliwa, Kristo Yesu, tutafufuka, amina, utukufu, katika nguvu na ufufuo wa Kristo, ndipo Uzima uliokuwa ndani ya Kristo utakuwa ndani yako, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Hiyo ndiyo shida. Naam. Hapo ndipo lilipo.

¹⁸³ Wanapataje dawa? Unajua jinsi wanavyopata dawa? Wanamchukua nungubandia, kisha wanatengeneza namna fulani ya vitu, dawa, na wanawazia hiki kinapaswa kufanya jambo fulani, nao wanakidungia nungubandia, na kama akipona, watakupa wewe. Mwajua, kila mtu hajaumbwa kama nungubandia, mwajua, wakati mwingine hiyo dawa itakuua. Kumekuwa na wengi waliouawa na penisilini kadiri ya walivyoponywa, ama, kusaidiwa. Kwa hiyo, mwajua, kila mtu hajaumbwa sawa, kwa hiyo itawasaidia wengine na kuwaua wengine, maana watu wote hawajaumbwa kama nungubandia. Lakini mnajua, itawasaidia wengine na kuwaua wengine, lakini kuna jambo moja la hakika, Dawa ya Mungu haitamdhuru mtu yeyote, bali itawaponya wote, hiyo ni kweli, kwa kuwa Yeye alisema, “Yeyote atakaye,” haitakuua, itakuponya. Loo, itawaponya waliovunjika moyo, iinue hiyo mikono dhaifu ipate kushangilia.

¹⁸⁴ Mchukue maskini mwanamke mfua nguo ambaye ni mshamba sana hata hawezi kuzungumza na mtu wa bima ajaye

mlangoni, na hebu ajazwe na Roho Mtakatifu, anaweza kutoa ushuhuda ambao utatikisa viezeko kutoka juu ya nyumba. Ana *kitu* fulani, jambo fulani limempata, amezaliwa katika Roho wa Mungu.

¹⁸⁵ Mchukue kahaba mwovu kuliko wote aliyewahi kutembea mtaani hapa nje, mbwa kamwe wasingemwangalia, hiyo ni kweli, mwache aingie na apate kusafishwa na Mungu, atakuwa na sifa njema kwa ujirani wowote. Sawa. Hivyo ndivyo neema ya Mungu ifanyavyo. Haipaki chokaa, bali inamsafisha akawa mweupe, hiyo ni kweli, inamnyosha kama mtutu wa bunduki.

¹⁸⁶ Ninaamini katika dini ya kale, ya huko nyuma msituni, ya anga la bluu, inayoua dhambi, naam, bwana, inayoua dhambi na ubinafsi, kisha unazaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, na kumwishia Yeye. Hiyo ndiyo inayokuokoa, ndugu.

¹⁸⁷ Wakati mwingine ninaporudi huko chini katika jimbo la Kentucky... Mnajua nini? Hao Wabaptisti huko chini katika jimbo la Kentucky wangepanya baadhi yetu Wapentekoste tuone aibu. Walisema, "Ndugu Branham, ulisema ati wewe ni Mbaptisti?" Naam, nilikuwa Mbaptisti halisi, hata hivyo, hatukupanda juu na kupeana mkono wa kuume wa ushirika, ndugu, tulishuka madhabahuni na kupiga-pigana mgongoni mpaka tukafaulu. Tulipoamka kutoka hapo, tulikuwa na *kitu*.

¹⁸⁸ Hivi majuzi huko California nilikuwa katika kanisa kubwa, moja ya makanisa yetu makuu ya Kipentekoste, na kufanya wito wa madhabahuni, ndipo watu watatu ama wanne wakaja madhabahuni, ndipo nikawasihi kwa dakika tano nipate mtu wa kuja aombe pamoja na hao wenye dhambi. Nilikuwa nimechoka sana, na kudhoofika, ilikuwa vigumu kwangu kusimama kutokana na kuhubiri, ndipo nikasema, "Je, kuna mtu atakuja kuomba?" Waliketi tu pale wagumu, lilikuwa ni kanisa la Kipentekoste. Vema, hao Wabaptisti huko chini wangewafanya waone aibu.

¹⁸⁹ Nilikuwa nikihubiri huko chini kwenye Siku ya Azimio, nyuma kabisa huko juu bondeni, nao maskini farasi walikuwa wakila mahindi kila mahali, chakula cha kutwa ardhini, Kutawadha-miguu, mwajua, na kusimama huko nje nikihubiri, nikihubiri juu ya *Tutafufuka, Haleluya, Tutafufuka Katika Asubuhi Ile Ya Ufufuo*. Nikasema, "Huyo hapo maskini nyanya yangu, nilimshika mikononi mwangu, mwenye umri wa miaka mia moja na kumi, wakati aliponikumbatia shingoni mwangu, kasema, 'Mungu aibariki maskini nafsi yako, Mpenzi,' akifa, 'milele. Nitakutana nawe Mbinguni.'"

Yapata wakati huo, maskini shangazi yangu akisimama huko nyuma, amevaa moja ya maskini hizo kofia ndefu, akasema, "Haleluya!" Huyu hapa anakuja, namna hiyo.

¹⁹⁰ Maskini mvulana mwenye dhambi amesimama pale ameshika kofia kubwa ya maganda mkononi mwake

namna *hiyo*, akasema, “Mungu, uirehemu nafsi yangu!” Naye huyu hapa anashuka kuja madhabahuni. Kabla hajafika pale, kulikuwako na karibu wale mama wa kale ishirini wamemzunguka, vema, aliokoka kabla hata hajafika madhabahuni, ndugu.

¹⁹¹ Mnataka kujua tulikula chakula cha kutwa saa ngapi? Yapata saa kumi na nusu alasiri hiyo. Ndugu, walikaa pale mpaka wakafaulu. Loo, walikuwa ni maskini Wabaptisti baridi, wa kawaida, sasa ni maskini Wapentekoste baridi, wa kawaida. Hiyo ni kweli, hivyo ndivyo tulivyo. Kweli kabisa.

¹⁹² Naam, wanampa maskini nungubandia dawa, wanampa, kama akipona, kisha wakupе, haitafaa kitu. Lakini mnajua, wakati Mungu alipokuwa tayari kujaribu dawa Yake, hakumpa nungubandia, alijipa Mwenyewe. Amina. Hiyo ni kweli, Mungu alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu kusudi aijaribu hiyo dawa Mwenyewe.

¹⁹³ Daktari yeyote mzuri kweli ataijaribu mwenyewe kabla hajampa mgonjwa wake. Hiyo ni kweli. Na Mungu, hiyo ndiyo sababu ilimbidi kufanyika mwili, Yehova alikuwa Roho, Mungu ni, Mungu Baba ni Roho; Mungu Mwana ni Mtu ambaye Roho wa Mungu aliishi ndani yake, sote tunajua hilo. Kwa hiyo basi wakati... Mungu alishuka na kufanyika mwili ili aweze kuinywa hiyo dawa.

¹⁹⁴ Kwa hiyo, kwenye kingo za Yordani, Yeye alijidunga hiyo sindano Mwenyewe, jambo kuu sana lililowahi kutukia, wakati nchi na Mbingu zilibusiana, wakati Mwana-Kondoo na Hua walipokutana. Hua, ndege mpole kuliko wote wa mbinguni. Mungu, Yehova aliji-... Mwenyewe, alijiwakilisha Mwenyewe katika ndege wa angani aliye mpole kuliko wote, hua; Mungu, Mwana, ambaye alikuwa ni Yesu Kristo, alijiwakilisha Mwenyewe katika mnyama mpole kuliko wote. Mwana-kondoo na hua, wote wawili wana asili moja.

¹⁹⁵ Vipi kama huyo Hua angeshuka juu ya mbwa mwitu? Angesema, “*Pshhh!* Siku za miujiza zimepita.” Huyu Hua *angeruka* amwache mara moja, hakika. Mara ya kwanza mbwa mwitu alipokoroma, akijua hizo hasira kali, mwajua, walikuwa namna hiyo, “Nitakwambia sasa hivi, kama wewe si mfuasi wa langu!” Loo-lo, Hua hakai hapo. Hua ni mpole, mwana-kondoo huongozwa.

¹⁹⁶ Mwana-kondoo hana ila kitu kimoja cha kutoa, hicho ni sufu.

¹⁹⁷ Nilimsikia mtu fulani akiniambia, kasema, mwanamke alisema, “Ni haki yangu ya Kimarekani kama nikitaka kuvuta sigara.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

Kasema, “Wanaiuza.”

198 Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa, lakini kama wewe ni mwana-kondoo, utapoteza haki zako, bali kama wewe ni mbuzi, hutafanya hivyo, kwa namna fulani, fanya tu lolote utakalo.” Unaona? Ni haki zako, bali unazipoteza kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Hiyo ni kweli. Unapoteza haki zako zote, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, unazipoteza, bila shaka.

199 Sasa, tunaona ya kwamba Mungu alichukua chanj-... Yeye Mwenyewe, dawa, alichanjwa. Walimwangalia maishani, walipomtemea mate usoni, Yeye hakusema chochote juu yake; wakati walipomvika tambara kuukuu, chafu kichwani Mwake, na kumpiga kichwani, kasema, “Sasa, kama wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga nasi tutaninii...” Yeye kamwe hakufungua kinywa Chake.

200 Walivuta makonzi ya ndevu kutoka usoni Mwake mpaka ukatokwa na damu, wakaweka taji ya miiba usoni Mwake. Akasema, “Ningeweza kusema na Baba Yangu, Naye angenitumia Mimi majeshi ishirini ya Malaika, lakini Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu.” Mnaona? Hiyo dawa ilishikilia wakati wa majaribu.

201 Walimpeleka msalabani, na kumwacha aone kiu pale juu, na afe, atokwe na damu mpaka mwili Wake wa kibinadamu ukauke, dawa ikashikilia. Hakujibu kwa hasira alipotukanwa. Ni dawa ya aina hiyo.

202 Kila mtu alikuwa, ulimwengu ulikuwa ukiiangalia, wanafunzi walikuwa wakiiangalia. Ndipo wakamwangalia mpaka hatimaye alipofikia ile saa ya mwisho, angesema nini? “Loo, nilikosea, nilikosea! Niondoeni, nitajiunga na makanisa yenu, nitaamini theolojia yenu!” Alisema, “Mikononi Mwako naiweka Roho Yangu. Baba, imekwisha.” Amina. Ee Mungu, hiyo dawa ilishikilia, ndugu, hiyo dawa ilishikilia.

203 Ndipo wakampa changamoto, baadhi yao wakasema, “Mdanganyifu huyu alisema ya kwamba angefufuka siku ya tatu. Hebu tuhakikishe.” Kwa hiyo wakachukua watu mia moja, wakabingirisha jiwe kubwa mlangoni, na kuweka muhuri wa Kaisari juu yake. Afadhali usiuvunje! Itakuwaje? Dawa iko wapi sasa? Utukufu kwa Mungu, kwenye asubuhi ya Pasaka, ilithibitisha ilichokuwa. Amina. Ilivunja muhuri wa Kaisari, ikavunja muhuri wa mauti, ikavunja muhuri wa kaburi, ikavunja muhuri wa kuzimu, ikafufuka tena, haleluya, imeshinda mauti, kuzimu, na kaburi. Dawa ya Mungu ilishikilia.

Kulikuwa na watu mia moja na ishirini waliosema, “Ninataka kuchanjwa, pia.” Ninataka chanjo ya namna hiyo, hivi hamtaki hiyo?

204 Yesu alisema, “Chanjo ile ile niliyo nayo, mtakuwa nayo, pia. Itafanya kazi juu yenu kama tu inavyofanya juu Yangu. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, iwapo tu mtachanjwa na Dawa hii ambayo nimecha-...”

“Mbona,” unasema, “hilo ni kosa.”

Loo, ngoja, sivyo pia, wawili walimjia, wakasema, “Bwana, jalia, mmoja wa wanangu aketi kwenye mkono Wako wa kuume, mwingine huo mwingine.”

Akasema, “Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho mimi? Mwaweza kubatizwa kwa ubatizo nibatizwao mimi?”

Kasema, “Naam.”

Kwa maneno mengine, “Kuchanjwa kwa chanjo ambayo nimechanjwa?”

Kasema, “Naam.”

²⁰⁵ Kasema, “Utafanya hivyo, lakini mkono wa kulia na wa kushoto si Wangu, huo ni wa Baba.” Lakini kasema, “Mtachanjwa,” kwa maneno mengine, “mtapokea kile kile nilicho nacho.”

²⁰⁶ Sasa, hivi hungetaka kuwa na chanjo hiyo? Hivi hilo si lingekuwa jambo zuri kujua ya kwamba ungeweza kuishi Maisha hayo, maishani ishara hizi zingekufuata, mautini ungeweza kusema, “Baba, imekwisha, mikononi Mwako naiweka Roho yangu”? Loo, jamani! Ndipo kwenye ile asubuhi ya ufufuo, utukufu kwa Mungu, huenda wakakupigapiga usoni kwa sepetu, lakini kwenye ile asubuhi ya ufufuo, utafufuka tena, kwa kuwa chanjo itashikilia. Waliiona imeshikilia katika saa ya kufa, ilishikilia katika majaribu, ilishikilia kwenye kitanda cha wagonjwa, ilishikilia kaburini, ilishikilia kuzimuni, ilishikilia kwenye Pasaka.

²⁰⁷ Na kulikuwa na mia na ishirini waliotamani chanjo hiyo, kwa hiyo wakaenda kwenye chumba cha juu kungojea chanjo yao. Amina. Yesu alisema, “Nitatuma Dawa ya chanjo ishuke mara tu mtakapofika kule na kungojea.” Loo!

²⁰⁸ Sasa ninaanza kujisikia kubarikiwa sana, kwa kweli najisikia. Utukufu! Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha kwa vyovyote vile, afadhali mwanze. Mnafikiri Wabaptisti hawapazi sauti? Huyu hapa mmoja anayepaza sauti, nami ninaamini hilo. Amina. Naam, ndugu. Haleluya! Akapanda kwenye vyumba vya juu, na kungojea ile chanjo ije. Mara ikaja Dawa ya chanjo kutoka Mbinguni.

²⁰⁹ “Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu?” Hii hapa chanjo inashuka, kile kisanduku cha matibabu kwa ajili ya uponyaji. “Kwa maana alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Haleluya! Dalili zilikuwa zimeyakabili mauti pale Kalvari, zikarudisha chanjo kwa Kanisa kwa ajili ya lile agizo, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waliopewa chanjo.”

²¹⁰ Kukaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, na kuwachanja watu mia moja na ishirini. Walitendaje? Ni kama tu ndama aliyetiwa chapa, ndugu hii hapa njia, wakiyumbayumba chini ya matokeo ya chanjo hiyo.

Ndugu, walikuwa wamelewa sana kwa Roho hata watu wakawazia walikuwa na kichaa, wakasema, “Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya.”

Petro akasema, “Ati tumelewa kwa divai mpya?” Akasimama na kuanza kuwahubiria.

²¹¹ Sasa, muda si muda mwajua, wakasema, “Tungependa kupata baadhi ya chanjo hii.” Waliona kitu halisi. Hao washiriki wa kanisa wenye njaa mioyoni waliona kitu halisi, Kitu ambacho kwa kweli hao watu walikuwa nacho kilikuwa kikiwafanya watende namna hiyo. Waliona ya kwamba walikuwa na Kitu, maana walionekana kana kwamba walikuwa walevi, na hata hivyo walikuwa wa kidini, na hata hivyo walikuwa na ishara zilizofuata. Kasema, “Vema sasa, mna daktari hapa? Kuna daktari yeyote hapa?”

Akasema, “Naam, tuna mmoja hapa, Dk. Simoni Petro. Njoo huku, Dk. Simoni Petro, waambie maagizo.”

Kasema, “Tufanye nini tupate kuokolewa? Tufanye nini tupate hiyo chanjo?”

²¹² Sasa, Petro akasema, “Vema, hamna budi kula mkate mwembamba. Hamna budi kupeana mkono wa kuume wa ushirika. Lazima ijaribiwe kwa miezi sita, kwanza, mwone kama kweli inafanya kazi au la.” Loo, rehema! Hiyo ni nadharia ya kujibunia.

²¹³ Petro alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Roho Mtakatifu.” Amina. “Kwa kuwa...” Labda alisema, “Ninawapa maagizo ya Milele.”

²¹⁴ Dk. Petro aliwapa ninii, Dk. Simoni Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, alitupa agizo la Milele, sio, “Kushikana mikono, kupeana mikono, kunyunyizia,” alisema, “Tubuni.” Sio, “Njoni mwingie kanisani,” bali alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, maagizo haya ni, yeyote atakaye, na aje.” Jambo ndilo hilo.

²¹⁵ “Je, hapana zeri katika Gileadi?” Hakika. “Huko hakuna matabibu?” Bila shaka. Hiyo ni kweli. “Basi kwa nini watu Wangu wangali wagonjwa?” Loo, haleluya!

²¹⁶ Mnajua kuna nini? Ukimwona daktari halisi ambaye ataandika maagizo, nawe uyapeleke kwa muuza dawa tapeli, naye aanze kuchanganya maagizo hayo, kitu kingine, atamwua mgonjwa. Kweli kabisa.

217 Hiyo ndiyo shida, tuna seminari nyingi mno za utapeli ambazo zimejaribu kufanya kitu kingine, “Jiunge na kanisa, mama yako ni mfuasi wa hapa. Andika jina lako kwenye kitabu.” Ndugu, usichezee agizo hilo, litoe kama tu vile daktari alivyoliandika. Haleluya! Basi matokeo yale yale yatakuja kama utafuata maagizo, usiyakwepe.

218 Sasa kumbukeni, maagizo yana *kiasi fulani* cha sumu ndani yake, halafu yana dawa ya kutosha kuivuruga sumu hiyo, sumu ya kutosha, anauchunguza ugonjwa wako, halafu anakupa dawa ya kutosha kuua hicho kijidudu, kiuasumu cha kutosha kuivuruga, isije ikakuua. Na kama ukiweka viuasumu vyote, havitakusaidia; ukiweka sumu yote, itakuua, kwa hiyo hayana budi kuwa ni maagizo yenye vyote viwili. Naye Mungu, yule Daktari, alijua jinsi ya kumpa Simoni Petro, naye akayaandika, kisha akasema, “Maagizo haya ni kwa ajili yenu, watoto wenu, na kwa hao walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

219 Sasa, mnasema Pentekoste si sahihi. Kuna shida gani? Unaenda kwenye duka la dawa la aina gani? Hiyo ndiyo shida, tuna michezo ya karata kanisani, michezo ya bahati nasibu ya kumlipa mhubiri, kuuza majogoo wa kale wa paani, karibu mnawachemsha, mnawauza kwa dola moja na nusu kwa sahani ili kumlipa mhubiri, huku amesimama pale juu akizungumza juu ya maua na kadhalika, na kamwe asihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kuna shida gani, ndugu? Hiyo ndiyo sababu tuna magonjwa, hiyo ndiyo sababu tuna watu ambao hawaamini katika uponyaji wa Kiungu, ni kwa sababu hawajachukua maagizo ya kweli. Amina.

220 Hebu upate ubatizo wa Roho Mtakatifu, nawe utaamini nguvu za Mungu, utaamini kila Neno analosema Mungu, utaliitikia kwa, “Amina,” kwa kila kitu asemacho Mungu.

221 Nao hao watu hawakuketi pale, na kusema, “Vema, Simoni, nadhani, *nadhani ni sawa*.” Ndugu, walipompokea Huyo, walijazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza kuyumbayumba kama walevi. Loo!

222 Pia kumbuka, ewe Mkatoliki, bikira Mariamu aliyebarikiwa alikuwa papo hapo. Na kama Mungu hangemruhusu aje Mbinguni bila yeye kuchukua maagizo yale yale, wewe utaendaje huko, na chochote pungufu? Baadhi yenu Wapentekoste baridi, wagumu, enyi Wabaptisti baridi, wagumu, ninyi Wamethodisti baridi, wagumu, mtafikaje huko, chochote pungufu ya hayo, wakati hata mama wa Yesu Kristo ilimbidi kwenda kule na kupata kitu kile kile, na kuyumbayumba, na kutenda kana kwamba alikuwa amelewa? Hiyo si Biblia, ninamwomba profesa yeyote aje na akalikanushe. Na kila wakati katika Biblia walipopata kumpokea Roho Mtakatifu,

walitenda jinsi hasa walivyotenda kule. Hayo maagizo yatakuwa na matokeo yale yale, wakati, kila wakati. Amina.

Ni saa ngapi? Loo! Nilidhani ilikuwa saa moja.

²²³ Loo, ndugu, sikiliza ndugu, sikiliza dada, kile ulimwengu unachohitaji leo ni kuona kitu halisi, hicho ndicho wanachotazamia, kuona kitu halisi, ninamaanisha watu halisi waliozaliwa mara ya pili.

²²⁴ Sasa, hao waliokusudiwa Uzima wa Milele wataliona, “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.” Kweli kabisa, hiyo ni kweli.

²²⁵ Mnasema, “Vema, naam, sisi ni Wapresbiteri sasa.” Ama “Sisi ni Wamethodisti, sisi...” Sijali wewe ni nani, kama ukisikia Sauti halisi ya Mungu, na Sauti halisi ya Mungu iliwafanya hao watu watende hivyo, na kufanya namna hiyo, na kuwa na huduma kama hiyo, nguvu zile zile za Mungu zitafanya jambo lile lile leo kama unaye. Hiyo ni kweli. Kama ulimpokea, atakutendea kama alivyowatendea. Bila shaka, ndivyo hivyo.

²²⁶ Petro alisema agizo hili ni kwa vizazi vyote, kwa hiyo ninyi watu mnaounda lundo la mafundisho ya sharti ya kujibunia na kuyaita *Fundisho*, mkiyaita kanuni za imani, kanuni za imani za kanisa, Presbiteri, Methodisti, Baptisti, na hata kanuni za imani za Kipentekoste, mna shida gani? Yachukueni maagizo ya Mungu.

²²⁷ Hiyo ndiyo sababu watoto ni wagonjwa, hawajatimiza agizo hilo bado. Mungu ana Zeri nyingi sana sasa, usijali kuhusu hilo, wewe tii tu hayo maagizo, uone kitakachotukia. Tubuni, mwone kama Roho Mtakatifu atakuja, mfanye kama Mungu alivyosema mfanye, mwone kama Roho Mtakatifu atakuja, mwone kama atakuwa na matokeo yale yale aliyokuwa nayo.

²²⁸ Kuna shida gani siku hizi, rafiki? Hatuna budi kuwa nayo kweli, hivyo ndivyo Mungu alivyosema, kitu kilicho *halisi*. Wakati nikizungumza kuhusu *halisi*, hebu nifunge. Mtanipa dakika tano zaidi?

²²⁹ Ninapenda kuwinda, ninapenda tu kuwinda, kutoka tu, na kuona machweo ya jua, na kuingia mwituni. Kama ninyi nyote mjuavyo, mama yangu ni chotara, mama ya mama yangu ametoka kwenye hifadhi za Wahindi, hupokea malipo ya uzeeni, mnaona. Kwa hiyo sisi... Kuongoka kwangu kamwe hakukuuondoa kwangu, kupenda mwitu.

²³⁰ Wafanyabiashara Wakristo, Full Gospel, hunipeleka kwenye Mto wa Kutorudi, kote ulimwenguni, Ninawinda huko Afrika, Asia, milimani. Bud Branham, Rainy Pass Lodge huko Anchorage, huyo ni binamu yangu, mnaona. Na ndege kumi na sita zikienda kuwinda dubu mkubwa mkali, kondoo, na kadhalika. Ninyi ndugu wawindaji, na kadhalika, mkiwahi kwenda huko juu, hebu nimwandikie, apate kuwaingiza huko

kwa bei nafuu. Mnaona? Kwa hiyo, na, nami huwa ninaenda huko juu na kufanya mikutano, nao wananipeleka bure, maana sina pesa zozote. Kwa hiyo, na hivyo ndivyo. . .

²³¹ Sababu ya mimi kutokuwa na pesa zozote, kama Bwana anataka kunituma Afrika, atasema, “Ndugu Branham,” mtu fulani atajitokeza, na kusema, “Bwana, alisema nikupe *hizi*.”

Ninasema, “Asante, Bwana, nilijua hilo,” *zoop*, ninaondoka.

²³² Mnaona, sina haja ya kuombaomba chochote, Bwana asipotaka niende, basi Yeye ananiweka hapa. Mnaona? Ninii tu, hiyo ndiyo njia ya kuishi, ninapenda kuishi hivyo, kile tu Yeye asemacho ni sawa. Sina chochote, sitaki chochote, kwa hiyo ninataka tu neema Yake, hivyo tu.

²³³ Nilikuwa nikiwinda kwenye misitu ya kaskazini, nilikuwa na mwindaji mwenzangu huko juu, nanyi, ninyi ndugu wote mnaowinda mnajua mwenzako mzuri wa kuwinda ni nini, mnafahamiana. Alikuwa mmoja wa wawindaji hodari sana, na shabaha bora sana niliyopata kuona, kamwe haikukubidi kumhofia. Wakati mwingine unamchukua zu—zuzu mwituni, na unakuta. . . Vema, *zuzu*, hilo linamaanisha “mshamba,” na ni neno la Kihindi. Lakini unampeleka mwituni, nawe itakubidi tu kumchungu, la sivyo atapotea. Lakini haikukubidi kuwa na wasiwasi juu ya maskini Bert, yeye alijua mahali alipokuwa, yeye mwenyewe alikuwa karibu nusu Mhindi.

²³⁴ Kwa hiyo, alikuwa ni jamaa mzuri, lakini mtu katili sana niliyepata kuona maishani mwangu. Alikuwa ni jamaa katili sana! Alikuwa akiwapiga risasi maskini watoto wa kulungu kusudi tu kunifanya nijisikie vibaya. Sasa, sidhani ni vibaya kumpiga risasi mtoto wa kulungu, kama hifadhi inasema umpige risasi mtoto wa kulungu, hilo ni sawa. Ibrahimu alimchinja ndama na kumlisha Mungu, kwa hiyo hiyo sehemu ya watoto wa kulungu ni sawa, bali sio tu kuwa katili. Ni ninii. . . si kile ufanyacho, ni jinsi unavyokifanya. Kwa hiyo wakati mwingine si kile unachosema, ni jinsi unavyokisema.

²³⁵ Na kwa hiyo basi huyu—maskini huyu mtoto wa kulungu, angewaona hao watoto, naye alijua, mimi nikiwa mhudumu mnajua, angewapiga tu risasi hao jamaa wadogo, wanane ama kumi wa hao kwa mwaka, ili tu kunifanya nijisikie vibaya.

Ndipo nikasema, “Bert, wewe ni mmoja wa marafiki wazuri sana, nami ninapenda kuwinda pamoja nawe kwa sababu wewe ni jamaa mzuri, lakini wewe ni katili sana.”

Akasema, “Ati unaniita katili?”

Nikasema, “Wewe ni zaidi ya hivyo, wewe ni mwovu.”

Naye akasema, “Ah, mhubiri, jirudie.” Kasema, “Wewe ni mwoga tu, kama wahubiri wengine.”

Nikasema, “Mimi si mwoga.” Lakini nikasema, “Jamani, wao . . . Mimi ni mwindaji,” kisha nikasema, “Si—sininii . . . Mimi si mwuaji, mimi ni mwindaji.”

Naye akasema, “Ah, rudia fahamu zako, Billy.”

²³⁶ Mwaka mmoja, huko juu, alisema . . . Nikakwea kule, nami nilikuwa nimechelewa kidogo kufika kule, msimu ulikuwa umefunguliwa majuma kadhaa. Na loo, kama mtu yeyote aliwahi kuwindia misitu ya kaskazini, hao mikia myeupe, loo, ndugu, nena juu ya Houdini, bingwa wa kutoroka, wao . . . na yeye ni—yeye ni mwanagenzi kwao wanaporushiwa risasi mara kadhaa, nao wa—wananinii tu, namna *hiyo*. [Ndugu Branham alidata vidole—Mh.]

²³⁷ Na wakati mwingine huwezi kuona umbali wa zaidi ya futi ishirini kutoka ulipo katika misitu hiyo kule Maine ambako wewe . . . A—afadhali ujue mahali ulipo, la sivyo hutarudi kamwe, kwa mamia ya maili ni tambarare tu, nawe unaanguka kwenye kinamasi, na kwenda juu ya kichwa chako mara kumi. Na—na ni uwindaji hatari tu. Kama wewe si mtu hodari wa mwituni, jiepupushe nao, isipokuwa uambatane na mtu fulani.

²³⁸ Kwa hiyo tulikuwa huko nje tukiwinda, nasi, na kabla hatujatoka nje . . . Mke wangu alikuwa pamoja nami, naye alikaa chumbani, kambini, na kuna yapata wanawake ishirini huko juu. Kwa hiyo mimi na Bert, daima tulivuka upande wa pili wa mlima, nasi tulijua mahali tulipokuwa, na tulikuwa tukiwinda, naye akasema, “Nina kitu fulani, Billy.”

Nikasema, “Ni kitu gani, Bert?”

²³⁹ Akaingiza mkono mfukoni mwake, naye alikuwa na filimbi ndogo. Angeweza kuipuliza, nayo ikasikika kama mtoto anayelia, huyo ni mtoto wa kulungu, mwajua, akimlilia mama yake.

Na, “Loo,” nikasema, “Bert, kweli wewe si katili hivyo. Vema, ungeninii . . . Kweli ungemwita mama kulungu kwa mlio huo wa mwana kulungu?”

Akasema, “Ah, rudia fahamu zako.” Kwa kweli sikuwazia angefanya hivyo, kweli.

²⁴⁰ Tukawinda, kulikuwako na yapata inchi sita za theluji uwanjani, karibu hizo, hali nzuri ya hewa ya kuwinda, kufuatilia, tuliwinda kote mpaka adhuhuri, hatukupata kitu, si hata mburuzo. Walikuwa, hao kulungu hula usiku, kisha mchana wanarudi chini ya vichaka na kadhalika, huwezi kuwasogeza. Na kwa hiyo, hawatasogea mpaka usiku uingie tena, isipokuwa umkanyage mmoja, umtoe nje.

²⁴¹ Kwa hiyo, basi tulikuwa tumewinda, yapata saa tano, saa tano na nusu. Na kila mara tulibeba chupa ya the—themosi iliyojaa chokoleti moto, na labda sambusa. Nasi tungepanda juu kadiri tulivyoweza, halafu adhuhuri tungekula, kisha tutengane,

naye angepitia njia nyingine nami njia nyingine. Nasi tungerudi kwenye hiyo kambi ya miiba usiku huo, tukaingia, labda saa nne ama saa tano usiku.

²⁴² Kwa hiyo basi, akaja kwenye uwazi mdogo wa ukubwa wa jumba hili la mikutano humu ndani. Naye kwa namna fulani tu, alikuwa mbele yangu, kwa hiyo kwa namna fulani alichuchumaa tu namna *hii*. *Chuchumaa*, nadhani hilo ni sawa hapa, sivyo? Wakentaki wa kutosha hapa wanajua ninalomaanisha ninaposema *kuchuchumaa*. Kwa hiyo kwa namna fulani aliinama tu chini, hasa, naye akaingiza mkono mfukoni mwake namna *hii*, naye alikuwa akitaka kuchukua ninii, akitaka kuchukua ninii yake, nilifikiri alikuwa akitoa sambusa yake, basi alipofanya hivyo, akatoa ile filimbi ndogo.

Ndipo nikamwangukia, nikasema, “Loo, aibu kwako, Bert!”

²⁴³ Akaipiga, nayo ikasikika kabisa kama mtoto mchanga akimlilia mamake. Basi alipofanya hivyo, niliangalia upande wa pili wa mahali hapo, ndipo kulungu jike mkubwa mno akasimama.

²⁴⁴ Naye alikuwa na macho kama tu ya mjusi, basi akaniangalia kwa hayo macho ya mjusi, namna *hiyo*, nami nikasema, “Loo, kweli hutafanya hivyo, Bert.” Nikasema, “Yeye, huyo ni mama, ndugu.” Nikasema, “Huyo ni mama, anafikiri tu huyo ni mtoto wake.”

Akasema, “Loo, jirudie, mhubiri.” Akanyemelea upesi *hivi* pamoja na bunduki yake.

Nikawaza, “Loo, jamani!”

²⁴⁵ Naye akaipiga tena. Ningeweza tu kuona hayo macho makubwa mno, na masikio makubwa yakitokeza namna *hiyo*. Hilo jike, mama kulungu, labda alikuwa na watoto, mnaona. Kwa hiyo, mtoto wake mchanga alikuwa katika shida, alikuwa akisikiliza, hayo masikio makubwa yameinuliwa juu. Na kwa hiyo, akaipiga tena. Sasa, hilo kabisa si la kawaida wakati huo wa mchana, saa tano mchana.

²⁴⁶ Kwa hiyo, akaingia moja kwa moja kwenye uwazi huo, sasa, hilo kabisa si la kawaida, kama mtu yeyote huwinda kulungu. Akatoka moja kwa moja akaingia kwenye uwazi huo. Shida ilikuwa ni nini? Alikuwa akimtafuta mtoto wake mchanga. Alikuwa akiangalia pande zote namna *hiyo*. Sasa, yeye hakuwa akiigiza sehemu ya mnafiki, alikuwa na kitu fulani ndani yake, alizaliwa mama, naye mtoto wake alikuwa katika shida, alikuwa akimtafuta mtoto huyo.

²⁴⁷ Mara tu nikamwona maskini Bert, kamwe hatubebi risasi kwenye—kwenye mtutu, na hiyo ni sera mbaya, kwa hiyo nikamwona akichukua hii .30-06 na kutia risasi hiyo ya uyoga ya chembe cha mia na themanini, loo, mlengaji hodari, akakivuta

kifuniko hicho chini, akakiinua namna *hiyo*, nazo hizo alama zilizopitana katika darubini hiyo papo hapo moyoni mwake.

²⁴⁸ Nikawaza, “Ee Mungu, mtu huyo anawezaje kufanya hivyo? Huyu mama akimtafuta mtoto wake mchanga, halafu awe katili vya kutosha kuulipulia mbali moyo huo mwaminifu wa thamani?” Mbona, upande wa pili wa jengo hili pamoja na hiyo, akitumia risasi hiyo nzito aliyo nayo, mbona, angeulipulia mbali moyo wake. Nikawazia, “Anawezaje kuwa katili hivi, ninii tu, kwa mama huyo wa thamani, huo moyo mwaminifu unaomtafuta mtoto wake mchanga, huko nje akimtafuta mtoto wake mchanga, kisha aulipulie mbali moyo wake?” Nikawaza, “Bert, wewe ni mwovu.”

²⁴⁹ Ndipo akaangalia chini, nikamwona akishuka chini namna *hii*, na kujiweka chonjo, na loo, ndugu, nilijua kitakachotukia. Nisingeweza kuliangalia. Na—na ninii... Nilipogeuka kuona kile alichokuwa akifanya, huyo kulungu alimwona yule mwindaji, naye akagutuka sana; hilo—hilo ni neno la mwindaji, hilo linamaanisha alishtuka sana. Naye a—akaangalia juu, akayatupa hayo masikio makubwa juu namna *hiyo*. Je, alikimbia? La, bwana. Kifo ama si kifo, mtoto wake mchanga alikuwa katika shida, alikuwa akimtatafuta. Loo, jamani! Asingeweza kujizua, alikuwa ni mama, alizaliwa mama. Hakuwa akiigiza sehemu ya mnafiki, alikuwa ni mama. Kifo ama si kifo, mtoto huyo alikuwa katika shida, naye alikuwa akimtafuta.

Ndipo nikawazia, “Hakika, hilo linapaswa kumgusa mtu huyo katili!”

²⁵⁰ Ninamwona akijiweka sawa, akijiandaa kupiga risasi. Nikageuza mgongo wangu, nisingeweza kuliangalia, kamwe nisingeweza kulivumilia, kumwona huyo mama wa thamani akienda kulipuliwa huo moyo mwaminifu wa thamani, kwamba alimpenda mtoto wake mchanga sana, hata alikuwa anaenda kulipuliwa huo moja kwa moja kutoka kwake. Akimwangelia, akimwangelia mwindaji, alikuwa ameketi pale, pia, huku anajua hiyo ilimaanisha kifo kwake, bali alikuwa akimtafuta mtoto wake mchanga.

²⁵¹ Ndipo nikageuka, nikawaza, “Ee Mungu, loo, anawezaje kufanya hivyo? Anawezaje kufanya hivyo? Jamani, katili sana!” Nilikuwa nimesimama nyuma ya msonobari mdogo, nikawaza, “Ee Mungu, anawezaje kufanya hivyo?” Kulikuwako na lundo la theluji pale. Nikawaza, “Mama huyo wa thamani atalipuliwa moyo wake moja kwa moja. Mungu, siwezi kuliangalia. Anawezaje kufanya hivyo?”

²⁵² Nikaona bunduki haikufyatuka, nikageuka kuona kile alichokuwa akifanya, alikuwa akienda *hivi*, alikuwa akienda, akitetemeka. Akageuka akaniangalia, macho hayo ya mjusti yalikuwa yamebadilika, machozi makubwa mno yalikuwa

yakitiririka mashavuni mwake. Akainyakua bunduki hiyo, akaitupa chini, akashika mguu wa suruali yangu, akasema, “Billy, yamenitosha, niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari zake kwamba ni halisi sana.”

²⁵³ Ilikuwa ni kitu gani? Aliona kitu halisi, aliona kitu ambacho hakikuwa maigizo, aliona kitu ambacho kilikuwa halisi, aliona upendo wa mama ambao ungesimama kuikabili mauti, ama haidhuru ilikuwa ni kitu gani, aliona kitu halisi, si mahubiri niliyohubiri, wala wimbo ambao kanisa liliimba. Yeye ni shemasi katika kanisa la Baptisti sasa.

²⁵⁴ Alinishika miguuni kwenye chungu cha theluji, akasema, “Billy, nimeona kitu ambacho ni halisi, mwanangu.” Kasema, “Yamenitosha,” kasema, “niambie habari Zake.”

Nikapiga magoti kwenye theluji, nami nikasema, “Bert, Mungu alisema, ‘Wakinyamaza, miamba hii itapiga kelele.’ Je, unampenda?”

Akasema, “Ninataka upendo kwa Mungu wangu kama ule kulungu huyo aliokuwa nao kwa mtoto wake mchanga.” Hapo kwenye chungu hicho cha theluji nikamwongoza mwindaji huyo kwa Mungu.

²⁵⁵ Sijui usiku wa leo, ni wangapi humu ndani wangetaka kuwa na upendo wa namna hiyo kwa Bwana wenu kama huo upendo halisi, halisi sana? Yeye, alifanya nini? Alionyesha kitu ambacho kilikuwa halisi. Sasa, enyi marafiki, kuna uigaji mwingi sana siku hizi, hebu tusiuchukue huo, hebu na tuwe na kitu halisi.

²⁵⁶ Muda umeenda sana, hebu na tusimame tu kwa miguu yetu, na kuyaweka maisha yetu wakfu kwa Mungu. Wote wanaotaka Mungu aingie moyoni mwenu, na kuwapa tukio la kuwa mpenzi wa Kristo, na umpende Kristo hata ungeweza kuikabili mauti ama chochote kile, upendo kama ule mama kulungu huyo alikuwa nao kwa mtoto wake mchanga, inueni mikono yenu namna *hii*. Na tuinamishe vichwa vyetu.

²⁵⁷ Naam, Bwana, tuna zeri, kuna zeri, kuna zeri katika Gileadi, huku kuna matabibu. Mungu, ninaomba ya kwamba utawasaidia watu sasa waje wakapewe chanjo, waje wakapate chanjo dhidi ya hasira, dhidi ya kutokuamini, wawe tayari kwa ajili ya ibada hiyo kuu, kesho. Tujalie, Bwana.

²⁵⁸ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, ni wangapi wenu wanaotaka upendo huo halisi wa Kipentekoste, wa Roho Mtakatifu wa Mungu? Hiyo ni Pentekoste, ni upendo halisi. Je, mwaweza kuja, msimame karibu na madhabahu ninapowaombea? Njoni, tokeni mahali mlipo sasa, huku mkisimama, njoni hapa sasa, na msemi, “Ninataka upendo wa namna hiyo, Ndugu Branham, nataka kumpenda Bwana wangu.” Mungu awabariki. Mungu awabariki. Hiyo ni kweli. Njoni kutoka kwenye roshani, tutangojea. Njoni moja kwa moja huku juu.

259 Hii huenda ikawa ndiyo saa ambayo yote kwa ajili ya Uzima...Ni kitu gani—ni kitu gani kilicho kikubwa zaidi kwako, rafiki? Haidhuru, kama wewe ni mfuasi wa kanisa, hilo halijalishi. Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa la Kipentekoste.” Lakini kama huna huo upendo wa kumfia Kristo kuuonyesha mbele ya ulimwengu, kusudi watu waweze kuona, si uje?

260 Ninyi Wapentekoste mnaojua ya kwamba mnaishi maisha, mna hasira, na mna fadhaa, na wakati mwingine mnaogopa, mna shaka, kwa nini msipande huku? Njoni huku, mwonyesheni Mungu kwa kuja tu hapa juu, “Sa—samahani, Mungu, na—na—na—nataka upendo, nataka upendo halisi, ninataka kukupenda Wewe, Bwana, kama yule mama kulungu alivyompenda mtoto wake mchanga.”

261 Unasema, “Lakini majirani zangu, mimi huenda kanisani pamoja nao.” Lakini Bwana wako, vipi kumhusu Yeye? Utakuja? Njoni kutoka roshani, sivyo? Kuna wengi wenu huko juu. Tutasimama papa hapa na kungojea.

262 Ninyi wanafunzi vijana hapa kutoka kwenye chuo hiki, mnatoka kwenda kuwa ndio wanaume wa kesho, wanawake wa kesho, mbona msije na kuyaweka maisha yenu wakfu? Hatuwaombi mjiunge na kanisa lolote la Kipentekoste, wewe dumu Mmethodisti, kile tu ulicho, lakini njoo upate tukio hili la upendo wa Mungu moyoni mwako, tamu sana, ili kwamba mkienda kwenye parokia yenu, popote Mungu atakapowaongoza, kijana mwanamume, kijana mwanamke... Mbona usije upate chanjo halisi kutoka kwa dhambi?

263 Baadhi yenu ninyi wanafunzi huko nje mnaovuta sigara, hivi hamna aibu? Njoni hapa. Mbona, John Wesley angepinduka kaburini mwake kama angalijua, wewe ukiwa ni mwanafunzi wake ukiwa na hizo. Njoni huku juu, sivyo? Bwana, mweke Mungu moyoni mwako, kweli. Njoni, hivi hamtakuja? Tokeni kwenye roshani, nyote, nyote, “yeyote atakaye,” maagizo yako wazi, usiku wa leo. Tuna zeri hapa Gileadi nao hawa hapa matabibu papa hapa, watawapeleka mkabatizwe, na chochote kile mkutanoni, tunao hapa. Hivi si mje? Hivi si mje mkajiweke wakfu tena kwa Mungu, na kupata tukio?

264 Mungu ataninii, sasa kumbukeni, Mungu atakuuliza, “Mbona hukuja?” Kabla ya asubuhi, kama ukishikwa na ugonjwa, usikie maumivu mikononi mwako, yakipitia karibu na mabega yako, unajua hiyo ni nini, sivyo? Unakufa. Ulihisi mapigo yako ya moyo yakipanda juu, mikono yako ikiingia baridi, daktari anakimbia kuja, anasema, “Ni mshtuko wa moyo.” Ambalansi inapiga king’ora, nawe ulihisi maisha yako, unabinya foronya, nawe unajua utakufa, Mungu atasema, “Mbona hukuja?”

“Vema, Bwana, nilikuwa mfuasi wa kanisa.” Hilo silo analozungumzia.

²⁶⁵ “Kwa nini? Kwa nini? Kwa nini bado kuna ugonjwa wa dhambi kanisani? Je, hapana zeri ya kuutibu?” Naam, kuna zeri ya kuutibu, huku kuna matabibu. Kila kitu kiko tayari, hivi si utakuja? Njoni sasa, wakati tuingojewa kwa muda kidogo tu.

... Mwokozi,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;

²⁶⁶ “Nifanye Mkristo, nifanye nizaliwe Mkristo, kama kulungu yule...” Huyu kulungu alikuwa nini? Alizaliwa mama, alizaliwa kuwa mama, njoo, ukazaliwe kuwa Mkristo. Njoo, utakuwa na upendo ule ule wa Mungu, zaidi sana kuliko yule kulungu aliokuwa nao kwa ajili ya huyo mtoto. “Mama aweza kumsahau mtoto wake mchanga anayenyonya? Naam, huenda akasahau, lakini siwezi kuwasahau,” alisema Yesu. “Jina lako limechorwa kwenye vitanga vya mkono Wangu.”

²⁶⁷ Hivi hutakuja? Ninakualika. Basi kumbukeni, kwenye ile Siku ya Hukumu mtakapoulizwa, “Kwa nini?” kanda iliyorekodiwa ya usiku huu itachezwa.

Usinipite.

Mwokozi...

²⁶⁸ Njoni, kila nafsi, kila nafsi, tabia, hasira, fadhaa, mashaka, wagonjwa, njoni. Kama huna imani ya kutosha kutii, hivi hutakuja sasa na kupata kitu halisi ndani yako kinachokupa imani? Unapanga kuponywa, kesho usiku, kwa nini usije sasa madhabahuni? Simama hapa, useme, “Bwana, niondolee mashaka yangu yote, chukua mashaka yangu yote, jalia kuwe na kitu hicho hapa kinachonifanya nijue kabisa. Nipe kitu ambacho, kesho usiku, wakati huo mstari wa uponyaji utakapoitwa, nitasema, ‘Bwana Mungu, hakuna kivuli cha shaka moyoni mwangu, ninakuamini Wewe, Bwana.’”

Unapozuru wengine,
Usinipite.

Mwokozi, Ee Mwokozi,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Loo, usinipite.

²⁶⁹ Angalieni, huku ameketi hapa pembeni, maskini mama akimnyonyesha maskini nanii wake—akimnyonyesha maskini mtoto wake mchanga pajani mwake. Kama mtu fulani angekuja, usiku wa leo, na kumwambia maskini mama huyo, “Nitakuua, ama huyo mtoto mchanga,” ni nani angekufa? Mama, hakika. Kwa nini? Huyu ni wake, alikaa chini ya moyo wake kwa muda wa miezi tisa, ni wake.

²⁷⁰ Kwa nini usikae chini ya moyo Wake sasa? Yakabidhi tu maisha yako Kwake. Yeye alikufa kwa ajili yako upate

kuokolewa, huu ndio ule upendo. Sasa, mama huyo angeweza, jambo fulani litukie kwake, naye angeweza kumsahau mtoto wake mchanga, Biblia ilisema hivyo, “Lakini kamwe siwezi kuwasahau,” Yeye alisema, “majina yenu yamechorwa katika vitanga vya mikono Yangu.” Hivi hamtakuja sasa? Hii ni, kama ibada ya kuweka wakfu, njoni sasa. Mara moja zaidi, nipate kuwa na hakika kwamba nilimwita kila mtu.

Sasa kumbukeni, ninyi Wakatoliki, mnasema, “Ndugu Branham, mimi ni Mkatoliki.” Sijali, Mkatoliki anaweza kuokoka kama chochote kile.

“Mimi ni Mbaptisti.” Vema.

²⁷¹ “Vema, mimi ni Mpentekoste.” Mpentekoste anaweza kuokoka kama tu mtu mwingine yeyote angeweza kuokoka, lakini kama huna... “Ingawa,” sikilizeni, “nijaposema kwa lugha za wanadamu na Malaika, wala sina upendo, si kitu mimi.” Hao ni Wapentekoste, wanene kwa lugha za wanadamu na za Malaika, lugha zinazojulikana, na zisizojulikana pia.

²⁷² Sasa, ninyi Wamethodisti, “Ingawa,” na Mbaptisti, na Wakatoliki, “nijapofahamu siri zote za Mungu, ninaweza kuielezea Biblia nzima, ninaijua yote, theolojia yangu ni ya hali ya juu sana, wala sina upendo wa aina hiyo, si kitu mimi. Nijapowapa maskini mali zangu zote, nitoe mwili wangu uhomwe moto kama dhabihu, imani ya kuhamisha milima, nijapoweza kufanya hivyo, wala sina upendo, si kitu mimi. Palipo na lugha, zitakoma; palipo na unabii, utabatilika; palipo na maarifa yatatoweka, bali upendo ujapo unadumu milele.”

Mpendwa Mwana-Kondoo anayekufa, Damu
Yako ya thamani
Kamwe haitapoteza nguvu zake,
Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa
Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

Sikilizeni:

Tangu wakati huo kwa imani nilipokiona hicho
kijito
Kinachosababishwa na majeraha yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio mada
yangu,
Na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa.
Kisha katika wimbo mzuri zaidi, mtamu zaidi,
Nitaimba nguvu Zako za kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu unaotetemeka,
unaogugumiza
Utakapolala kimya kaburini.

²⁷³ “Jalia niishi ndani Yako kwa kila wakia ya nguvu zangu, mwili wangu, na yote niliyo mimi kuonyesha upendo wa Yesu Kristo uliomiminwa ndani ya mioyo yetu na Roho Mtakatifu.”

²⁷⁴ Sasa kila mtu humu ndani, ninyi mlio karibu na madhabahu, chochote kilicho shida yako, kiungame kwa Mungu, “Nina hasira. Ninazo tabia. Ninayaonea aibu maisha yangu. Nimefanya *hili, lile*, ama *linginelo*.” Nitawaombea, ninataka kila mtu awe na kicho.

²⁷⁵ Baba yetu wa Mbinguni, watu hawa wamekuja juu ya Neno rahisi la Mungu aliye hai, na juu ya hadithi iliyotukia yapata miaka ishirini iliyopita, wakati mwindaji mwenye moyo katili, kuwa katili na asiyejali, siku hiyo huko juu ya chungu hicho cha theluji, alipomwona mama kulungu akionyesha upendo halisi, wa kweli, aliona kitu halisi, hilo ndilo alilotaka. Hakika, kama Mungu angeweza kumpa mnyama upendo wa namna hiyo, angeweza kumpa mwanadamu. Hapo ukampa hilo tukio kuu la kuzaliwa mara ya pili.

²⁷⁶ Sasa, Baba, hawa wanaosimama madhabahuni, ni wanawake, kina mama, baba, watoto, Mungu, wamesimama hapa tayari kuupokea upendo huo. Jalia wasije hapa juu bure, lakini jalia wadhamirie sana kwamba watachanjwa kutokana na uovu wao, mawazo yao, fadhaa za—za—zao, hasira zao, hata Roho Mtakatifu atakapowashukia, Bwana, kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Tujalie, Bwana. Kupitia Jina la Yesu Kristo, ninawakabidhi Kwako.

Sasa, ninawatakeni ninyi makasisi, mpande juu hapa karibu nao, mumwendee kila mmoja...?...

Hawa hapa wahudumu, wakipanda hapa juu kupiga magoti na kuomba.

²⁷⁷ Sasa, kila mtu katika kusanyiko inamisha kichwa chako, wakati nikimwomba Ndugu Borders kama atatuongoza katika maombi.

²⁷⁸ Ninawakabidhi kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwa ajili ya shauku ya moyo wenu iliyowaleta hapa, tunapoomba. 

61-0413 Kwa Nini?
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org